
# **150** wajitokeza upandikizaji wa mimba, gharama zake zapunguzwa

UKURASA 3




# **IDU** yataka katiba mpya kabla uchaguzi wa mwaka 2025

UKURASA 3


Nipashe Spotika
NUKUU YA DECLAN RICE WA ARSENAL, UKURASA 13
MAMBO MAWILI MBAPPE ANAWEZA KUIPA MADRID
ISIKUPITE

UKURASA 11

Nipashe

Jumatatu Julai 17, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581374

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

## RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Mjamzito aliyebakwa apoteza pacha wake

• **MADAKTARI** wathibitisha vichanga kufia tumboni, watumia saa tisa kukitoa kichanga cha pili... *Ukurasa 4*

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

### MUME AUAWA AKIMWOKOA MKEWE SHAMBULIO LA FISI



MKAZI wa Kijiji cha Chiwambo, Kata ya Lulindi, wilayani Masasi, mkoani Mtwara, Haika Mangeja (62), amefariki dunia baada ya kuvamiwa na fisi wakati akijaribu kumwokoa mke wake...

UKURASA 2

### Simba aliyetoroka hifadhini ajeruhi askari-pori, auawa



Askari wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) wakiwa wamempakia simba jike waliyemuua katika kijiji cha Iramba Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa jana. Wa pili kushoto ni askari Joachim Mafuru aliyejeruhiwa na simba huyo. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi (katikati), akishuhudia utiaji saini wa mkataba wa mkopo wa ushirikiano wenye thamani ya dola milioni 200 kati ya Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto) na Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Dk. Juma Malik Akili (kulia), jana Unguja. **Habari uk. 17. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia asema mmomonyoko maadili ugonjwa wa taifa

UKURASA 2

**MICHEZO** **MAZOEZI YA YANGA USIPIME** UK.24 **MAONI** UK.6



Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, akizungumza kwenye mkutano wa hadhara katika uwanja wa stendi ya sokoni Zingiziwa, Chanika, Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Samia asema mmomonyoko wa maadili ugonjwa kwa taifa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema mmomonyoko wa maadili nchini ni ugonjwa unaoliandama taifa na jamii inaathirika na ukatili wa kujinsia, wizi na dawa ya kulevya - mambo yanayoitia aibu nchi, familia na jamii.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akifungua Kongamano la Wanawake wa Kiislamu Zanzibar na maadhimisho ya Mwaka Mpya wa Kiisilamu.

Alisema matendo hayo yanadhalilisha, kuondoa heshima na haiba ya nchi huku yakisababisha vijana wengi 'kupotea', lakini jamii imeyaacha hadi kufikia kiwango hicho.

"Ukiangalia kwa undani kwanini tumefika hapa, ni ukosefu wa elimu ya msingi ya dini. Tungekaa wote tukajua dini inasema nini, vijana wetu wakaelimishwa dini inasema nini, imani, makatazo tusingefikia hapa, tungeharibikiwa lakini sio kiasi kikubwa namna hii.

"Kama wazazi tujiulize tumefikaje huku? Tufikishe elimu tuliyoipata, ili iwe ni chachu ya hamasa ya kusimamia maadili mema ndani ya familia, tuweke msingi kwa watoto kuchukia tabia mbaya wanazoziona kwa wazazi na walezi wetu," alisema.

Rais Samia alisema watoto wanapoona matendo ya wazazi na walezi wakisengenya watu wanasikiliza, au wanaposutana, kuzodoana, kuzusha bila ushahidi, wanajifunza tabia zisizo njema, jambo ambalo linawaharibu.

Pia alisema mwanamke ana mchango mkubwa kiuchumi, kijamii na kisiasa huku akiwataka wawe na elimu ya dini na dunia, ili waisaidie jamii kuepuka vitendo viovu kwa kuwa bila elimu ni ngumu kumwokoa yeyote.

"Kwenye kitabu cha Quran kimeonyesha wanawake 11 walitoa mchango wao kusimamisha dini, kuchangia kiuchumi, wakati wa vita walitoa mali watu wakaenda vitani, wakaachiwa miji, wakaongoza na kulisha miji. Hii inaonesha uwezo mkubwa wa mwanamke, tunakwama wapi? Ninaomba tujitafakari,"alisema.

Rais Samia alisema kuwa hata sasa wanawake wamekuwa mstari wa mbele kupigania haki, kushiriki katika mambo ya kitaifa na jamii kwa kufanya mambo na kazi ambazo huko nyumba zilionekana si za mwanamke.

"Nikiangalia hapa ninaona tupo wanawake viongozi wengi, mawaziri, wakurugenzi, wabunge, wake wa viongozi ambao tunatoa mchango wa maana kwenye taifa lakini tunakwama, tunarudishana nyuma, unyanyasaji unarudisha nyuma maendeleo," alisema.

**MALALAMIKO UTENGUZI**

Rais Samia pia alisema ndani ya serikali hufanyika tathmini ya wanaofanya vizuri na vibaya kwa kutambua mchango wa kila mmoja. Wanapoondolewa na kuwa wa imani moja, kelele ni nyingi lakini "mabadiliko lazima yaume".

"Tustahimili kuumia kwa mwanao kuondoka, mdogo wako kuondoka ili taifa linyooke, vinginevyo tunyooshane tangu nyumbani, anayepewa dhamana asiwe na tamaa, uzembe.

"Sisi wakubwa hatuwezi kuvumilia hayo, tuna mambo mengi ya ndani na kimataifa tunataka wasaidizi wetu watusaidie lakini unamwona fulani nikimweka hapa atafanya vizuri kuliko aliyepo, nikimwondoa yanatokea manung'uniko, ya nini? Hebu tuache hizi kelele, tuwape viongozi fursa za kujenga taifa," alisema.

Rais pia alisema kila anayeishi Zanzibar ni Mzanzibar. Ana haki sawa na mwingine, na anayeoonekana anafaa ndiye atakayewekwa.

"Nianze kwa kujiusia mwenyewe maana pale Mungu alikoniweka siyo haba, na ukisikiliza ya watu ni mtihani mkubwa sana. Tushiriki na tuige mifano mizuri tutakayooneshwa na viongozi wa dini katika kutumia njia bora na hekima katika kuendesha maisha yetu," alisema.

Rais Samia aliwataka watu kuchunga ndimi katika kuongoza wengine na kuacha tabia za kujikweza, bali watangulize busara, hekima na kama kuna hoja asaidiwe na kuelekezwa.

"Unakosa nini ukimweleza mtu, tukipewa madaraka tunapandisha mabega kama mizani, tupo juu, wanaume makoti yananing'inia, shungi ziko juu.

Hii siyo kabisa. Tunapoona familia fulani imeharibika tuelekezane kwa wema na sio kuwasengenya," alisema.

Rais pia alisisitiza wananchi kulinda amani na utulivu wa taifa, akisisitiza"...tukiwa na amani, utulivu wawekezaji watakuja. Tukiparurana hawatokuja.

"Nilimsikia Mkurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji (TIC) anasema tumepokea wawekezaji wengi kuliko nyakati zingine kwa sababu kuna amani. Tutunze amani na utulivu. Tunapotofautiana suluhu ipatikane, tukae vizuri ili mambo yaendelee," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema uhusiano mzuri uliopo kwa viongozi wakuu wa nchi ndicho kichocheo cha maendeleo yaliyopo.

Katibu Mtendaji Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar, Khalid Mfaume, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuhakikisha wanahamasisha jamii na wananchi kujua kalenda rasmi la Kiislamu.

# Simba aliyetoroka hifadhini ajeruhi askari-pori, auawa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

ASKARI-PORI amejeruhiwa usoni na mguuni wakati akimuua mmoja wa simba wanaotishia maisha ya wananchi wa wilayani Kilolo mkoani Iringa baada ya kutoroka hifadhini.

Katika Uwanja wa Luganga wilayani Kilolo ambako samba aliyeuawa alikuwa ameletwa ili wananchi wamwone jana, Kamishna Msaidizi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania(TAWA), Joachim Makwai, aliwaambia waandishi wa habari kuwa matukio ya simba yalianza Juni 13 mwaka huu, wanyama hao waliposhambulia mifugo.

Alisema kuwa kutokana na matukio hayo kuendelea kuwa tishio, askari wa TAWA walianza ufuatiliaji wa karibu na kuweka mitego katika maeneo yote ambayo simba wamepita na kuua mifugo.

Makwai alisema simba hao waliua nguruwe katika Kijiji cha Iramba wilayani Kilolo ndipo askari walipoweka mtego ambako walikuwa wakilala na kufanikiwa kuwakamata.

Alisema kuwa TAWA, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) na madaktari wa mifugo walifanikiwa kumnasa mmoja wa simba hao. Ilikuwa ngumu kumfikia kwa ajili ya kumlaza kwa sindano ya usingizi ndipo walipolazimika kutumia bunduki.

"Eneo ambalo simba jike huyu alikuwa amenasa ni sehemu ya ardhi oevu na ilikuwa vigumu kumfikia kumchoma sindano ya kumlaza ili kumkamata akiwa hai ndipo tulipoamua kutumia risasi kwa kumpiga na kutokana na kutaka kujiokoa alimrukia askari wetu mmoja na kumjeruhi usoni japo tayari alikuwa hana nguvu kutokana na risasi alizokuwa amepigwa," alifafanua Makwai.

Alimtaja askari aliyejeruhiwa kuwa ni Charlesy Mafuru kutoka TAWA, ambaye baada ya kujeruhiwa alikimbizwa Hospitali ya Wilaya ya Kilolo ambako alipatiwa matibabu na kuruhusiwa. Makwai alisema wanaendelea kuwasaka simba wengine, akibainisha kuwa wanyamapori hao wamegawanyika katika makundi mawili - kuna simba aliyekuwa katika Kijiji cha Maboga, Jimbo la Kalenga ambako inasadikika alirudi Hifadhi ya Taifa Ruaha (RUNAPA) baada ya matukio ya mifugo kuuawa kutotokea tena ila kundi la pili ni hilo la aliyeuawa jana.

Aliwataka wananchi kuendelea kuwa waangalifu zaidi hasa nyakati za jioni na usiku, ni muda wa simba kuwinda.

Diwani wa Dabaga, Joseph Tengelapo, alisema kuwa kabla ya simba huyo kuuawa, alikuwa ameua mbuzi, ng'ombe na nguruwe katika vijiji vya kata anayoiongoza.

Askari aliyejeruhiwa na simba, Joachimu Mafuru, alisema kuwa asubuhi walifanikiwa kwenda eneo ambalo walitega mtego huo akiwa na askari wenzake watano na baada ya kufika eneo la mtego walisikia ngurumo za simba lakini hawakujua eneo sahihi alikokuwa.

Hivyo, walipotawanyika kumtafuta, askari wenzake walifanikiwa kumpiga risasi kifuani na wakati simba akijaribu kujitetea ndipo alipokutana naye uso kwa uso akitaka kumrukia. Akajiokoa kwa kumfyatulia risasi mfululizo kifuani hadi alipoanguka chini. Alisema kupona kwake kumetokana na nguvu ya bunduki aliyotumia (SMG).

"Hili ni tukio langu kubwa la pili kunusurika kifo dhidi ya wanyama. Lingine ambalo sitolisahau ni la kupambana na nyati aliyejeruhiwa. Nilifanikiwa kumuua," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, aliwapongeza askari hao kwa ujasiri walioonesha, akiungana na wananchi kuwachangia Sh. 500,000 kama zawaida. Wananchi walichanga kiasi kingine na kuwa na zawadi ya Sh. 640,000.

## HABARI KITAIFA




Daktari wa Macho, Dk. Joseph Sungura, kutoka Hospitali ya CCBRT akimhudumia mmoja wa wananchi waliofika katika banda la CCBRT katika kampeni ya upimaji afya ijulikanayo Afya Check mwishoni mwa wiki kwenye viwanja vya Barafu Mburahati jijini Dar es Salaam. Kampeni hiyo imeandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kushirikiana na Afya Check ya Clouds Media Group. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# IDU yataka katiba mpya kabla ya uchaguzi 2025

**Na Jenifer Gilla**

BARAZA la Uongozi la Umoja wa Vyama vya Kidemokrasia Duniani (IDU), limeitaka Serikali ya Tanzania kuurejesha mchakato wa katiba mpya, ili kuleta mabadiliko makubwa yatakayowezesha maendeleo shirikishi.

Vilevile, limeitaka serikali kufanya mabadiliko ya mifumo ya sheria zote za kitaasisi zinazohusika na uchaguzi ili kuwapo na uchaguzi huru, wa haki na unaokubalika kabla ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) jana, IDU imetoa tamko hilo kupitia azimio lake maalum lililoangazia hali ya siasa na demokrasia nchini, katika kilele cha maadhimisho ya miaka 40 ya kuanzishwa kwa baraza hilo, jijini London, Uingereza.

IDU imeitaka serikali kuhakikisha nchi haiendi katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, kabla ya kufanya mabadiliko makubwa ya katiba na kisheria juu ya uendeshaji wa uchaguzi ili kuzuia wizi wa kura katika uchaguzi.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa baraza hilo pia limepokea uamuzi wa nchi kuondoa zuio la mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa kwa tahadhari na kutaka kufutwa kwa sheria kandamizi zilizotungwa katika serikali ya iliyopita. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kilele cha maadhimisho hayo kilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo mawaziri wakuu wastaafu, Boris Johnson wa Uingereza, John Howard na Morison Scott wa Australia na Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje wa Marekani, Michael Pompeo.

# 150 wajitokeza kupandikiza mimba

**Na Elizabeth Zaya**

ZAIDI ya watu 150 wamejitokeza kutafuta huduma ya kupandikiza ujauzito katika Kituo cha Afya cha Huduma za Upandikizaji cha India (CFC) kilichoweka banda katika maonesho ya Sabasaba yaliyomalizika Julai 13 mwaka huu.

Balozi wa CFC Tanzania, Shose Kombe, alimwambia mwandishi wa habari hizi kuwa wengi waliotembelea katika banda lao, walikuwa na shida ya kupata watoto na hivyo walitaka kupatiwa elimu ya namna ya kupatiwa huduma hiyo ya upandikizaji.

"Mwaka huu tuliamua kuja kushiriki katika maonesho haya kwa sababu tumekuwa tukipata Watanzania wengi wanaokuja India kwa ajili ya kufuata huduma hii ya upandikizaji watoto.

"Tulianza na maonesho ya Diamond na tukaona tuunganishe na haya ya Sabasaba kutokana na mwitikio mkubwa wa watu kuhitaji huduma hii.

"Kituo chetu tangu kianze kutoa huduma hii kimekuwa mkombozi mkubwa kwa wengi wenye shida ya watoto. Kwa hiyo, katika kupanua wigo wa utoaji huduma hiyo, tumeshiriki katika maonesho haya," alisema.

Aliongeza kuwa lengo la kushiriki maonesho hayo ni kutoa elimu kwa wanaokumbana na tatizo la uzazi.

"Na hili ni kwa wale ambao wanatafuta watoto wa kuongeza na hawajapata kwa muda mrefu na wale ambao hawajawahi kupata kabisa na ni kituo ambacho kimevunja rekodi ya kuzalisha watoto kwa njia ya upandikizaji. Zaidi ya watoto 50,000 wamezalishwa katika kituo hiki tangu kianze kutoa huduma hii," alisema Shose.

"Tumekuja Tanzania katika maonyesho kwa sababu tunapata wagonjwa wengi kutoka Tanzania na ambao wengi wamefanikiwa. Kwa hiyo, tukaona tuje ili kuwaelimisha zaidi. Na tumeweka punguzo kubwa sana kutokana na hali ya uchumi licha ya kuwa huduma hii ni ghali sana. "Tumepunguza hadi dola za Marekani 2,000, sawa na Sh. milioni 4.6 na lengo letu kubwa ni kusaidia watu na si kupata faida. Na huduma zetu zinapatikana India. Kwa hiyo, tunaweka punguzo ili mtu amudu," alisema.

# Benki yaja na hatua mpya utoaji huduma

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Standard Chartered Tanzania imesisitiza dhamira yake ya kuchangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini huku ikikasimu kwa Access Bank Plc kutoa huduma za wateja, kampuni binafsi na biashara za kibenki (CPBB).

Standard Chartered na Access Bank Plc (Access) zilitangaza Ijumaa kuingia makubaliano ya uuzaji wa hisa za benki hiyo katika kampuni tanzu za Angola, Cameroon, Gambia na Sierra Leone na biashara yake ya kuhudumia wateja, kampuni binafsi na biashara za kibenki.

Maandalizi ya mabadiliko haya yalianza Aprili 2022 wakati benki ilipoamua kimkakati kupanua wigo wa huduma zake katika nchi kadhaa zikiwamo Lebanon, Angola, Cameroon, Gambia, Sierra Leone, Zimbabwe na Jordan.

Nchini Tanzania, benki itaondoka na kutoa huduma za CPBB inayojulikana pia kama shughuli za benki kwa wateja wadogo na kujikita zaidi kutoa huduma kwa kampuni na taasisi.

Kwa mujibu wa taarifa ya benki hiyo iliyosambazwa kwa vyombo vya habari jana, makubaliano na Access kwa uuzaji wa biashara ya benki hiyo Kusini mwa Jangwa la Sahara yanaendana na mkakati wa kimataifa wa Standard Chartered, unaolenga kufikia ufanisi wa utendaji kazi, kupunguza utata na gharama za uendeshaji.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa Benki ya Access itatoa huduma mbalimbali za kibenki na mwendelezo kwa wadau wakuu wakiwamo wafanyakazi na wateja wa biashara za Standard Chartered katika nchi zilizotajwa hapo juu.

Taarifa hiyo ilibainisha kwamba benki ya Access na Standard Chartered zitafanya kazi kwa karibu katika miezi ijayo ili kuhakikisha mabadiliko ya haraka, huku shughuli hiyo ikitarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 12 ijayo.

Akizungumzia makubaliano hayo, Herman Kasekende, Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania, Standard Chartered, alisema: "Tumekuwapo Tanzania kwa zaidi ya miaka 106 na tunaamini kwa dhati mustakabali wa maendeleo wa muda mrefu wa nchi hii chini ya makubaliano haya.

"Access Bank itafanya biashara ya CPBB Tanzania pekee. Inasubiri idhini za udhibiti na utekelezaji wa mauzo, tungependa kuwahakikishia wateja wetu kwamba bidhaa zetu zote, huduma na mifumo ya benki itafanya kazi bila matatizo na makubaliano yetu na Access Bank."

Alisema benki hiyo inaamini kuwa imepata matokeo mazuri kwa kutafuta mshirika bora kwa ajili ya biashara zake zenye maslahi kwa wafanyakazi wake pia.

Kufuatia taarifa hilo, alisema benki hiyo itaendelea na shughuli zake nchini. Itawafahamisha wateja wake juu ya mchakato mzima.

Alisema Benki ya Access ina kiwango, ujuzi na anwai ya bidhaa inayotakiwa katika kipindi hiki cha mpito cha kuhamisha shughuli zake.

Benki hizo mbili zitafanya kazi kwa karibu ili kuhakikisha muda wa mpito unakuwa mzuri kwa wateja pasipo usumbufu.

Access Bank ni kampuni tanzu inayomilikiwa kikamilifu na Access Holdings Plc na benki inayoongoza ya huduma kamili ya kibiashara inayofanya kazi kupitia mtandao wa matawi na vituo vya huduma zaidi ya 600, ikijumuisha mabara matatu, masoko 18 na wateja milioni 52.

**KIWANJA KINAUZWA**

**KIWANJA KIPO KISUKURU** SEGEREA **JKT DSM,** KINA UKUBWA WA MITA ZA MRABA **(SQM) 2252,** KIWANJA KIMEPIMWA KINA HATI, **BEI MILIONI 60.** KWA MAWASILIANO: **0754 857523, 0655857523**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MTWARA**
**ILIYOPO MTWARA**
**(EXTENDED JURDICTION)**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 24/2019**
**(Asilia shauri la jinai Na. 1/2014, Mahakama ya Wilaya ya Mtwara)**
**MKURUGENZI WA MASHTAKA....................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**MUSSA MALYANGO BUSOGO & WENZAKE.............MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: MUSSA MALYANGO BUSOGO–KIMARA KILUNGULE – DSM**
**GERDAT LUKAS MMUNI – KONGOWE – DSM**
**HAMIDU ABDALLAH NGUNDE – MTONI KWA AZIZI – DSM**
**BONIFANCE KOSAINI BUSOGO – KIMARA KOROGWE – DSM.**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MTWARA KUSIKILIZA RUFAA HII MNAMO TAREHE 20/7/2023 SAA 3:00 ASUBUHI BILA KUKOSA.

KUMBUKA KKUKWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA BASI RUFAA HII ITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO.

IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 5/7/2023.

F. R. LUKUNA
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Mjamzito aliyebakwa apoteza pacha wake

## -Madaktari wathibitisha vichanga kufia tumboni

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa**
MKURANGA



MJAMZITO aliyebakwa wiki sita zilizopita, amekumbana na kilio kipya. Ujauzito wake uliothibitika kuwa ni wa pacha umeharibika. Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Dk. Ally Mbikilwa amethibitisha.

Usiku wa tarehe 5 Juni mwaka huu, mama huyo, mkazi wa Mtaa wa Kazole, Kata ya Vikindu wilayani Mkuranga, mkoani Pwani, alibakwa na hatimaye kufungwa katika kiroba.

Alikimbikizwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga usiku huohuo.

Dk. Mbikilwa, alipotakiwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Dk. Gunini Kamba, kutoa ufafanuzi kwa mwandishi wa habari hizi Ijumaa iliyopita, alithibitisha Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga kutoa matibabu kwa mama huyo.

Alirejea historia ya matibabu hayo kwamba, Juni 5 mwaka huu walipompima kwa ultrasound baada ya kubakwa, walibaini alikuwa na ujauzito wa wiki 24 na alipofikishwa kwao usiku wa kuamkia Julai 12 mwaka huu, akihisi uchungu, walimpima tena kwa kipimo hicho na kubaini ujauzito ulikuwa umefikisha wiki 28 (miezi saba).

Dk. Mbikilwa alifafanua kitaalamu kwamba, ili mtoto kuwa timamu, mama anatakiwa kubeba ujauzito kwa wiki 37 hadi 38, hivyo kwa tukio la mama huyo wa Vikindu, kuumwa uchungu katika juma la 28 ni tatizo.

"Mtoto wa kwanza alitolewa tumboni saa 10 alfajiri. Uzito wake ulikuwa gramu 900, yaani hata kilo moja alikuwa hajafikisha. Akaendelea kupewa dripu ya uchungu kumsaidia kumtoa mtoto wa pili.

"Saa saba mchana (Julai 12 mwaka huu) akatolewa mtoto wa pili. Alikuwa na uzito mdogo zaidi - gramu 700. Mama aliruhusiwa kutoka hospitalini jana (Julai 13 mwaka huu).

Anatakiwa kurejea tena baada ya siku saba kwa ajili ya kuangalia maendeleo yake.

"Kwa hiyo, kitaalamu watoto wamekufa katika wiki ya 28 tumboni. Kwa namna vipimo vilivyoonesha, ni wazi kwamba wakati wa mama kubakwa, wale waliombaka walimwumiza tumboni. Kwa hiyo, wale watoto walikufa katika mazingira hayo," alifafanua.

Dk. Mbikilwa alibainisha kuwa miili ya watoto ilikuwa na majeraha na hata kuoza katika baadhi ya maeneo. Alitaja hali hiyo imetokana na ama kukandamizwa au kupigwa.

"Mpaka wanatolewa tumboni, walikuwa wameshaharibika. Kama binadamu nimeumizwa na tukio hili.

Kama ningekuwa ninasimamia sheria, na nimewapata hao wahalifu, aah ningewahukumu kifungo cha maisha gerezani," Dk. Mbikilwa alisema.

Mwandishi alipohitaji ufafanuzi kuhusu muda wa saa tisa aliotumia mama huyo kusubiri kutolewa tumboni mtoto wa pili (kutoka saa 10 alfajiri hadi saa saba mchana) na hatari yake kiafya, Dk. Mbikilwa alisema:

"Kwa ujauzito uliokamilika (wiki 37 hadi 38), watoto pacha wanapaswa kupishana kuzaliwa siyo zaidi ya nusu saa. Ikitokea unapita muda huo elekezi, basi inabidi upasuaji ufanyike, vinginevyo kuna hatari ya kumpoteza mama na mtoto.

"Sasa, suala la huyu mama ni tofauti - watoto walikuwa hawajafikia muda wa kuzaliwa. Kilichofanyika kwake ni kutoa vile viumbe tumboni. Lakini kwa kipindi chote cha kusubiria kumtoa mtoto wa pili, mama alikuwa chini ya uangalizi wa madaktari."

Katika hilo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Dk. Kamba, alisema: "Madaktari waliotoa huduma kwa huyo mama, walikuwa na hatua tatu za kuchukua; kumsubiri atoe mtoto kwa njia ya kawaida ya kusukuma ambayo ni salama zaidi; kumfanyia upasuaji ambao ungemsababishia kidonda; au kuingiza vifaa vya kukatakata hicho kiumbe na kutoa kipande kimoja baada ya kingine.

"Ninafikiri uamuzi uliochukuliwa wa kusubiria mama asukume, ulikuwa sahihi japo inaonekana amesubiri kwa muda mrefu (saa tisa) hadi kutolewa mtoto wa pili."

Mume wa mama huyo (jina tunalo) alimwambia mwandishi wa habari hizi kwamba, alisaidiwa na majirani wanne (wanawake watatu), kumpeleka mkewe hospitalini Mkuranga, wakitumia gari la jirani yao.

"Tulitoka hapa nyumbani saa tano usiku. Tulipofika hospitalini, majirani wakatuacha huko, wakarudi nyumbani. Wataalamu baada ya kuangalia kadi ya kliniki ya mke wangu, walionekana kushtuka.

"Wakasema afanyiwe kipimo cha ultrasound ili kuangalia usalama wa watoto. Yaliyoendelea usiku huo sikujua maana sikuruhusiwa kuingia katika wodi ya wazazi," alisimulia.

Mkewe anaeleza kilichojiri wodini usiku huo kwamba, alipopimwa ilibainika watoto walikuwa wamefia tumboni. Ni taarifa aliyopewa zikiwa zimepita siku 36 tangu alipobakwa chumbani kwake na hatimaye kufungwa katika kiroba na kupoteza fahamu kwa saa saba.

Kwa mujibu wa mama huyo, hatua iliyofuata baada ya kuarifiwa watoto wamefia tumboni, aliwekewa dripu ya maji ya uchungu na ilipotimia alfajiri (Julai 12 mwaka huu), mtoto wa kwanza (wa kiume) alitolewa.

Anamwelezea kwamba, kichwa chake kilikuwa kimeharibika, kikiwa na ishara za kuoza.

Anasema kuwa baadaye mchana siku hiyo, mtoto mwingine (wa kike) alitolewa tumboni, naye akiwa si riziki. Mama huyo anaeleza kuwa mkono wa kulia na sehemu za siri za mtoto huyo zilikuwa zimeoza.

Anabainisha kuwa tangu alipokumbana na ukatili wa kubakwa Juni 5 mwaka huu, kulitokea mabadiliko katika kucheza kwa watoto tumboni.

"Walipunguza kucheza tumboni. Kulikuwa na uchungu unakuja kisha unakata. Yaani ninajihisi kama uchungu lakini unapotea ghafla. Hii ya juzi usiku (Jumanne) nilihisi kama uchungu hivi. Nikajihisi kama ninataka kwenda hajandogo, nikaenda msalani - haitoki, haja kubwa haikutoka.

Halafu vikaja vichomi vya uchungu wenyewe ninaoujua; nikajua kabisa huu ni uchungu (ni mara ya nne kwake kubeba ujauzito).

"Nikamwambia mume wangu kwamba ninajisikia uchungu. Akaenda kwa jirani yetu mwanajeshi, ana gari. Yule mwanajeshi (mwanamke) akamwita dereva wake wakatupeleka hospitalini. Tulisindikizwa na majirani wengine wawili (wanawake).

"Tulifika hospitalini saa saba usiku. Nilikuwa nina uchungu lakini kuzaa sizai. Wakanipeleka chumba cha ultrasound. Wakanipima, wakasema 'tunaona watoto wawili ila hawako hai'.

"Hapo ndipo sasa nikawekewa dripu ya maji ya uchungu. Mtoto wa kiume alitolewa usiku. Mwingine alitolewa mchana (Julai 12 mwaka huu) baada ya kuhangaika sana, nikihudumiwa na madaktari wanawake.

Hata yule aliyenisaidia kusukuma mtoto wa pili ni daktari mwanamke, alikuwa amevaa nguo za kijani," mama huyo anafafanua.

Anafafanua zaidi kwamba "nimelazwa hospitalini kwa siku mbili. Nimeruhusiwa kutoka leo (Alhamisi iliyopita) mchana. Lakini kabla ya kuruhusiwa, walimtaka dada yangu alipie Sh. 27,000, vinginevyo sitolewi hospitalini. Akalipa.

"Wakahitaji kujua historia ya ujauzito wangu. Nikawaambia matatizo yote yaliyotokea dhidi yangu. Wakaniruhusu kutoka hospitalini saa saba mchana."

Kuhusu hili la mjamzito kutakiwa kulipia huduma za uzazi hospitalini Mkuranga, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Dk. Mbikilwa, alitoa maelezo haya kwa mwandishi:

"Hatutozi huduma ya uzazi. Huduma zote za uzazi huwa ni bure. Kama kuna huduma amelipishwa huyo mama, basi ni kipimo cha ultrasound ambacho gharama yake ni Sh. 25,000, maana hana bima. Huduma zingine za uzazi hapa ni bure."

Mnamo Julai 3 mwaka huu, Nipashe ilichapisha ripoti kuhusu tukio la kubakwa mjamzito huyo na kufungwa katika kiroba huko Mtaa wa Kazole, Kata ya Vikindu wilayani Mkuranga.

Ni uhalifu uliofanywa usiku wa Juni 5 mwaka huu dhidi ya mama huyo wa watoto watatu wenye umri wa miaka 13, tisa na mitano. Yeye ana umri wa miaka 36.



Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Dk. Gunini Kamba

# Mahakama yaamuru mfanyabiashara kurejesha umiliki wa hisa kama awali

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Biashara imetoa amri dhidi ya mfanyabiashara Jiteshi Jayantilal Ladwa, ikitaka umiliki wa hisa na ukurugenzi wa Kampuni ya Indian Ocean Hotel Limited, urejeshwe kama ilivyokuwa kabla ya Aprili 16, 2020.

Amri hiyo ya Mahakama imetolewa mbele ya Jaji Dk. Deo Nangela kutokana na maombi yaliyowasilishwa na wanahisa wenza wa kampuni hiyo, Dhirajilal Walji Ladwa, Chandulal Walji Ladwa na Nilesh Jayantilal Ladwa, baada ya kukubaliana na hoja za waombaji kupitia kwa mawakili wao, Patrick Kaheshi na Robert Rutaihwa kama walivyoomba.

Baada ya kusikiliza maombi hayo, mahakama iliamuru hali ya kampuni kuhusiana na umiliki wa hisa na ukurugenzi irejeshwe kama ilivyokuwa kabla ya Aprili 16, 2020.

Amri ya pili, mahakama imemzuia Jitesh, wawakilishi wake na watu aliowaajiri katika kampuni hiyo kutokuchukua hatua zozote zinazoweza kuingilia mchakato unaolenga kutatua mgogoro unaohusu umiliki wa hisa na ukurugenzi wa kampuni hiyo. Wasubiri kumalizika shauri lililofunguliwa na wanahisa wenza.

Tatu; mahakama imemwelekeza msajili wa kampuni kuhakikisha kuwa hali ya kampuni hiyo ilivyokuwa awali kabla Jitesh kubadilisha taarifa zake kwa kujihamishia na kujimilikisha hisa za wanahisa wenza inadumishwa na jambo lolote lililofanywa na Jitesh linabadilishwa na kutoa taarifa za utekelezaji.

Jitesh ni mmoja wa wanahisa katika kampuni mbalimbali zinazomilikiwa kwa ubia na wanafamilia ya Walji Ladwa, jijini Dar es Salaam, ikiwamo Indian Ocean Hotels Limited, inayomiliki hoteli maarufu ya Golden Tulip Masaki, akiwa na hisa 15.

Wanahisa wengine katika kampuni hiyo ni Dhirajilal (asilimia 40) na Chandulal (asilimia 30) ni baba zake wadogo na mdogo wake Nilesh Jayantilal ambaye ana hisa 15.

Kumbukumbu zilizoko mahakamani, zinaonyesha Jitesh amekuwa na mgogoro na wanahisa wenzake, akidaiwa kutumia nguvu kuwazuia wenzake kuingia katika ofisi za kampuni hizo akiwatumia walinzi wa Suma JKT.

Kutokana na hali hiyo, wanahisa wenzake hao wamemfungulia kesi mbalimbali ikiwamo kesi ya kibiashara namba 2 ya mwaka 2020, waliyoifungua Januari 20, 2020, wakipinga Jitesh kuwaondoa katika menejimenti ya kampuni hiyo ya Indian Ocean na kuwazuia kuingia katika ofisi za kampuni hiyo.

Hata hivyo, wakati tayari hatua muhimu za kisheria zikiwa zimeshasikilizwa ikiwamo usikilizwaji wa hoja za kisheria alizoziibua Jiteshi katika pingamizi dhidi ya kesi hiyo Aprili 16, 2020, Jitesh alibadili umiliki wa hisa za kampuni hizo.

Anadaiwa kuwa alijihamishia hisa za wanahisa wenzake hao akidai kuwa amezinunua kutoka kwa wanahisa hao, kwa bei ya Sh. 40,000 kwa kila hisa.

Msajili wa kampuni alikubaliana naye na kufanya mabadiliko ya taarifa za kampuni hiyo kupitia mfumo wa usajili mtandaoni (ORS) wa Brela ikiwamo umiliki wa hisa pamoja na wakurugenzi.

Wanahisa hao baada ya kupata taarifa hizo ndipo wakafungua shauri hilo dogo namba 62 la mwaka 2020, wakiomba amri hizo kusubiri kusikilizwa na kutolewa uamuzi kesi ya msingi.

Shauri hilo lilisikilizwa kwa njia ya maandishi na Jitesh aliwalilishwa na Wakili Jeremiah Mtobesya, alipinga maombi hayo, akidai kuwa uhamishaji wa hizo za wanahisa wengine ulifanyika kihalali.

Katika uamuzi wake, Jaji Nangela alisema shauri hilo dogo halihusiana na kuhamishwa au kutokuhamishwa kwa hisa kama wakili wa Jitesh alivyodai, bali uhalali wa yale aliyoyafanya Jitesh wakati tayari kuna shauri mahakamani.

Jaji Nangela alisema alichokifanya Jitesh kilikuwa ni makosa na cha kuchukiza kwa kuzingatia kwamba tayari wadaiwa walikuwa mahakamani na kwamba ni matumizi mabaya ya taratibu za kimahakama.

"Kwa hoja hizo, chochote kilichofanywa katika mfumo wa usajili wa kimtandao wa Msajili wa kampuni ni batili na hayana maana kisheria. Katika mazingira hayo, amri ya kumrejesha hali ilivyokuwa kabla ya Aprili 16, 2020, inatakiwa na ni ya maana na ya haki," alisema Jaji.

# Kinana akoshwa wizara mpya

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, amepongeza uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kuunda wizara inayohusika na mipango.

Pia amepongeza hatua ya kuifanya Tume ya Mipango kuwa chini ya Ofisi ya Rais, akiamini itaongeza kasi na uhakika wa mipango ya maendeleo nchini.

Kinana aliyasema hayo jana wilayani Kibiti mkoani Pwani wakati wa mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mbunge wa Jimbo la Kibiti, Ally Mpembenwe, ukiwa na ajenda ya kueleza utekelezaji wa Ilani ya CCM.

"Hivi karibuni Rais ameunda wizara mpya inayoshughulika na mipango, kwa lugha nyingine ni Tume ya Mipango ambayo ipo ofisini kwake, lengo lake moja tu - tumekuwa tukifanya mambo mengi nchi hii lakini bila mipango mizuri.

"Rais akaona wizara ile inapoitwa Wizara ya Fedha na Mipango inafanya kazi zaidi ya kukusanya na kutumia kuliko kupanga, akaona hapana! Ninadhani ni vizuri sasa tutengeneze wizara ya mipango," alisema.

Aliongeza: "Rais katika uzoefu wake akaona hapana, hakuna maendeleo bila ya mpango, hakuna mapato bila mpango, hakuna matumizi bila mpango.

Kwa hiyo, wizara hii na tume hii itakapoanza kazi ninawahakikishia Watanzania maendeleo yatakuwa ya uharaka zaidi kuliko ya sasa na kuliko mlivyowahi kuyaona."


airtel

A REASON TO IMAGINE

**MUONGOZO WA GHARAMA ZA AIRTEL KUANZIA JULAI - SEPTEMBA 2023**

**LIPIA KADRI UNAVYOTUMIA: KODI IMEJUMUISHWA**

| | | Bei (TSh) |
|---|---|---|
| MITANDAO YOTE | TSh / sek | 0.50 |
| NDANI YA MTANDAO | TSh / sek | 0.50 |
| INTANETI | TSh / Mb | 9.35 |
| SMS ZA NDANI YA NCHI | TSh / Sms | 8.00 |
| SMS ZA NJE YA NCHI | TSh / Sms | 215.00 |

**MITANDAO YOTE**

| Muda | Bei(TSh) | Mitandao Yote (Dak) | SMS |
|---|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 30 | 25 |
| Saa 48 | 1,000 | 150 | 25 |
| Siku 7 | 1,500 | 150 | 50 |
| Siku 7 | 2,500 | 300 | 50 |
| Siku 30 | 5,000 | 400 | 100 |
| Siku 30 | 10,000 | 1,200 | 100 |

**BANDO ZA SMS**

| Muda | Bei(TSh) | SMS |
|---|---|---|
| Saa 24 | 200 | 200 |
| Siku 7 | 500 | 1,000 |
| Siku 30 | 1,000 | 10,000 |

**BANDO ZA INTANETI**

| Muda | Bei (TSh) | Intaneti (MB) |
|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 245 |
| Saa 24 | 1,000 | 490 |
| Siku 3 | 2,000 | 985 |
| Siku 7 | 2,000 | 950 |
| Siku 7 | 2,100 | 1,024 |
| Siku 7 | 3,000 | 1,434 |
| Siku 7 | 5,000 | 2,460 |
| Siku 30 | 10,000 | 4,608 |
| Siku 30 | 20,000 | 9,800 |
| Siku 30 | 30,000 | 14,750 |
| Siku 60 | 50,000 | 24,600 |
| Siku 60 | 100,000 | 49,200 |

**BANDO ZA AIRTEL - AIRTEL**

| Muda | Bei (TSh) | Ndani ya Mtandao (Dak) | Mitandao Yote (Dak) | SMS |
|---|---|---|---|---|
| Saa 24 | 500 | 90 | 10 | 25 |
| Saa 48 | 1,000 | 260 | 40 | 25 |
| Siku 7 | 1,500 | 260 | 40 | 50 |
| Siku 30 | 5,000 | 1,000 | 250 | 100 |

**COMBO (DAKIKA + MB)**

| Muda | Bei (TSh) | Mitandao Yote (Dak) | SMS | Intaneti(MB) |
|---|---|---|---|---|
| Saa 24 | 1,000 | 40 | 10 | 350 |
| Siku 7 | 2,000 | 55 | 10 | 800 |
| Siku 30 | 10,000 | 400 | 10 | 3,600 |
| Siku 30 | 20,000 | 500 | 10 | 8,192 |

**BILA KIKOMO**

| Muda | Bei (TSh) | Mitandao Yote (Dak) | SMS | Intaneti (MB) |
|---|---|---|---|---|
| BILA KIKOMO | 1,000 | 30 | 50 | 10 |
| BILA KIKOMO | 2,000 | 20 | | 900 |

**MUONGOZO WA GHARAMA ZA KIMATAIFA (KODI HAIJAJUMUISHWA)**

| Nchi | BAND | Bei(TSh/Sek) |
|---|---|---|
| China, Canada, India, USA | Band 1 | 8 |
| Malaysia, Japan, Lebanon, Ethiopia, Nigeria, Pakistan, Yemen, Sudan, Kenya Airtel, Kenya Other Network, United Arab Emirates | Band 3 | 10 |
| REST OF AFRICA, Denmark, Germany, Ireland, Netherlands, Norway, Spain, Sweden, Oman, Italy, Ghana | Band 5 | 14 |
| Zambia, Dem. Rep. of Congo, Zimbabwe, Burundi, Malawi | Band 6 | 25 |
| France, Rest of World, South Africa, United Kingdom | Band 7 | 13 |
| Central African Republic, Sao Tome & Principe, San Marino, Montenegro, Cuba, Martinique, East Timor, Nauru, Papua New Guinea, Solomon Islands, Vanuatu, Wallis & Fatuna, Cook Islands, Kiribati, Tuvalu, Micronesia, Maldives, South Sudan, Comoros, Gambia, Latvia, Somalia, Bulgaria, Lithuania, Moldova, Albania, Belarus, Congo, Guinea, Guinea Bissau, Seychelles, Sierra Leone, Senegal, Samoa, Tonga, Uzbekistan, Vanautu, Cameroon, Chad, Gabon, Madagascar, Belgium, Switzerland | Band 8 | 47 |
| Uganda , Uganda celtel, Rwanda | Band 11 | 15 |
| Satellite, Inmarsat, Premium Diego Garcia, Ascension Island, St.Helena, GreenLand Falkland Islands, Tokelau, Dem. Rep. Of Congo, Special numbers, Chile, Australia Territories, Niue Island, Upt, Norfolk Island, Chile | Band 12 | 233 |

| BANDO ZA KIMATAIFA | MUDA | BEI YA BANDO (TSH) | DAKIKA |
|---|---|---|---|
| INDIA, CHINA, USA CANADA | Saa 24 | 1,000 | 20 |
| AFRIKA KUSINI | Saa 24 | 3,000 | 5 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Saa 24 | 2,500 | 5 |
| ULAYA | Saa 24 | 2,500 | 4 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Saa 24 | 2,500 | 3 |
| INDIA, CHINA, USA CANADA | Siku 7 | 5,000 | 100 |
| AFRIKA KUSINI | Siku 7 | 6,000 | 10 |
| MALAWI, DRC | Siku 7 | 10,000 | 8 |
| ZAMBIA | Siku 7 | 10,000 | 9 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Siku 7 | 5,000 | 10 |
| UK, ITALY, GERMANY | Siku 7 | 5,000 | 8 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Siku 7 | 5,000 | 6 |
| INDIA, CHINA, USA CANADA | Siku 30 | 15,000 | 300 |
| AFRIKA KUSINI | Siku 30 | 15,000 | 25 |
| MALAWI, DRC | Siku 30 | 20,000 | 16 |
| ZAMBIA | Siku 30 | 20,000 | 18 |
| MASHARIKI YA KATI (UAE,Saudi Arabia,Yemen,Lebanon,Pakistan & Qatar ) | Siku 30 | 15,000 | 30 |
| UK, ITALY, GERMANY | Siku 30 | 15,000 | 24 |
| AFRIKA MASHARIKI (Uganda Kenya & Rwanda), OMAN | Siku 30 | 15,000 | 18 |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | Dakika za kupiga simu | Dakika za kupokea simu | MB |
|---|---|---|---|---|---|
| Eneo -1 | Siku 3 | 10,000 | 5 | 5 | 75 |
| Eneo -1 | Siku 7 | 25,000 | 15 | 10 | 250 |
| Eneo -1 | Siku 14 | 40,000 | 25 | 20 | 500 |
| Eneo -2 | Siku 3 | 25,000 | 12 | | 250 |
| Eneo -2 | Siku 7 | 50,000 | 15 | | 200 |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo -1 | Saa 24 | 5,000 | 500 |
| Eneo -1 | Siku 3 | 10,000 | 1,299 |
| Eneo -1 | Siku 7 | 15,000 | 2,048 |
| Eneo -1 | Siku 14 | 30,000 | 5,120 |

**SAFARI ROAMING BANDO - KUPIGA NA KUPOKEA SIMU**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | Dakika za kupiga simu | Dakika za kupokea simu |
|---|---|---|---|---|
| Eneo -2 | Siku 7 | 10,000 | 10 | |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo -3 | Siku 3 | 40,000 | 1024 |
| Eneo -3 | Siku 7 | 70,000 | 2048 |
| Eneo -3 | Siku 14 | 200,000 | 5120 |

**SAFARI ROAMING BANDO - INTANETI**

| Bando kwa nchi | Muda | Bei ya Bando (TSh) | MB |
|---|---|---|---|
| Eneo - 4 | Siku 3 | 35,000 | 200 |
| Eneo - 4 | Siku 7 | 90,000 | 512 |
| Eneo - 4 | Siku 14 | 175,000 | 1024 |

| | |
|---|---|
| Eneo 1 | Kongo B(Airtel), DRC(Airtel), Gabon(Airtel), Ghana(Airtel),Kenya(Airtel), Madagasca(Airtel), Malawi(Airtel), Niger(Airtel), Nigeria(Airtel), Rwanda(Airtel), Seychelles(Airtel), Tchad(Airtel), Uganda(Airtel), Zambia(Airtel), India(Airtel) & Mauritius(Emtel) |
| Eneo 2 | **AFRIKA:** Botswana(MTN), KongoB(Airtel), KongoDRC(Airtel), Egypt(Orange), Gabon(Airtel), Ghana(Airtel), Kenya(Airtel), Madagascar(Airtel), Malawi(Airtel), Mauritius(Emtel), Mozambique(Vodafone), Niger(Airtel), Nigeria(Airtel), Rwanda(Airtel), Afrika Kusini (MTN, Vodafone), Swaziland(MTN), Tchad(Airtel), Uganda(Airtel), Zambia(Airtel) |
| | **MAREKANI:** (T-Mobile) & CANADA: (Bell, Telus) |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** China(China Mobile), Bangladesh(Airtel), India(Airtel), Israel(Pelephone, Cellcom), Oman(OmanTel), Pakistan(Telenor, Vimplecom), Qatar(Qtel), SaudiArabia(Zain), SriLanka(Airtel), Turkey(Vodafone), UAE (dU, Etisalat) |
| | **ULAYA:** Denmark(Telenor, TDC), France(Orange, SFR), Germany(T-Mobile, Vodafone), Greece(T-Mobile), Italy(Vodafone,Tim), Netherlands(Vodafone, KPN), Norway(Telenor), Romania(Vodafone, Orange), Russia(Vimpelcom), Spain(Vodafone, Telefonica), Sweden(Telenor), UK(Vodafone,Telefonica) |
| | **OCEANIA**: New Zealand(Vodafone) |
| Eneo 3 | **AFRIKA:** Botswana(MTN), Cameroun(Orange), Egypt(Orange), Ghana(Airtel, TIGO), Mali(Orange), Mozambique(Vodacom), Mauritius(Emtel), Senegal (Orange), Swaziland(MTN), Afrika Kusini(MTN, Vodacom) |
| | **MAREKANI:** (T-Mobile) & CANADA: (Bell, Telus) |
| | **ULAYA:** Belgium(Base, Orange), Switzerland(Swisscom), Denmark(Telenor, TDC), France(Orange, SFR), Germany(T-Mobile, Vodafone), Greece(Cosmote), Italy(Vodafone,Tim), Netherlands(Vodafone, KPN), Norway(Telenor), Romania(Vodafone, Orange), Russia(Vimpelcom), Spain(Vodafone, Telefonica), Sweden(Telenor), UK(Vodafone,Telefonica) |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** India(Airtel), Israel(Orange, Pelephone, Cellcom),Pakistan(Mobilink, Telenor), Qatar(Qtel), SaudiArabia(Zain), Sri Lanka(Airtel), Turkey(Vodafone), UAE(Etisalat) |
| | **CHINA:** China Mobile |
| Eneo 4 | **AFRIKA: Afrika Kusini**(Cell C) |
| | **MAREKANI:** AT&T |
| | **MASHARIKI YA KATI NA ASIA YA KATI:** Oman (OmanTel), UAE (dU), Turkey (Turkcel) |

*Vigezo na masharti kuzingatiwa. Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea tovuti yetu: https://www.airtel.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TPLB mulikeni sasa ubora wa viwanja Ligi Kuu Bara

**SHIRIKISHO** la Soka nchini (TFF), kupitia Bodi yake ya Ligi (TPLB), limetanga msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/24 utaanza rasmi Agosti 15, mwaka huu, ikiwa ni siku mbili tu baada ya mchezo wa fainali wa Ngao ya Jamii kuchezwa katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Ikumbukwe msimu huu Ngao ya Jamii itashirikisha timu nne za juu kwenye Ligi Kuu kwa mtindo wa mtoano, Yanga ikicheza dhidi ya Azam FC na Simba ikivaana na Singida Fountain Gate FC, ambapo washindi wa mechi hizo watakutana fainali Agosti 13, mwaka huu.

Hata hivyo, kuelekea msimu mpya, karibu timu zote 16 zitakazoshiriki Ligi Kuu msimu wa 2023/23, tayari zipo katika maandalizi ya msimu mpya huku zikiendelea kuboresha vikosi vyao kwa kufanya usajili baada ya dirisha hilo kufunguliwa tangu Julai Mosi huku likitarajiwa kufungwa Agosti 31, mwaka huu.

Kwa usajili unaoendelea kufanywa na klabu 16 zitakazoshiriki ligi hiyo pamoja na maandalizi zinazofanya, tunaamini ligi itakwenda kuwa ngumu na upinzani utaongezeka maradufu ya msimu uliopita ambao ulimalizika kwa Yanga kuwa mabingwa.

Hata hivyo, wakati huu klabu zikiwa katika maandalizi makubwa, tunatamani pia kuona wamiliki wa viwanja wakivifanyia ukarabati mapema ili ligi itakapoanza wachezaji waweze kuonesha viwango vyao.

Si hilo tu, bali ubora wa viwanja utaongeza ushindani mkubwa pamoja na kuvutia mashabiki wengi kwenda viwanjani, jambo ambalo limekuwa kilio kikubwa si tu kwa klabu bali na TFF pia ambayo imekuwa ikisuguа kichwa na kufanya utafiti kujua kinachopungaza mashabiki viwanjani.

Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sasa ni ya tano kwa ubora barani Afrika, na kwa namna ushindani na uwekezaji unavyoongezeka na kuzidi kuvutia wachezaji wengi kuja kucheza soka nchini, tunaona ipo nafasi ya kupanda juu zaidi.

Hivyo, ili kuwezesha kupiga hatua zaidi hakuna njia ya mkato zaidi ya viwanja kuendelea kuboreshwa hususan eneo la kucheze kama ambavyo sheria namba moja ya Fifa inavyotaka.

Katika hilo tunasisitiza na kuitaka TFF kupitia TPLB, kuweka mkazo mkubwa katika maboresho ya viwanja mapema na isisite kuvifungia vile ambavyo havitakuwa vimekidhi viwango stahiki.

Tunatambua imekuwa kawaida kwa baadhi ya wamiliki wa viwanja kuviboresha mwanzoni mwa msimu na baada ya kuchezwa mechi tatu hadi tano, hushindwa kuendelea kuvitunza na kuharibika kabisa kiasi cha kuilazimu TPLB kuvifungia.


Kwa mantiki hiyo, tunaikumbusha TPLB zoezi la ukaguzi wa viwanja kufanyika sasa na kuwa endelevu kwa kufanyika angalau kila baada ya raundi mbili za ligi, hilo litasaidia kuwafanya wamiliki kutolala na kuvihudumia kila mara.

Matarajio yetu ni kuona kila timu inaanza na kumalizia ligi katika uwanja wao nyumbani bila kukutana na adhabu ya kufungiwa kutokana na ubovu, kwani hilo likitokea zitakosa sapoti kubwa kutoka kwa mchezaji wao wa 12 ambaye ni mashaki.

Aidha, kwa kuwa viwanja vingi vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM), tunakikumbusha pia kuvikarabati ili kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuendeleza sekta ya michezo nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Mkude ndiye mwenye uamuzi pekee kuagwa Simba ama la

**KUMEKUWA** na sintofahamu kubwa kwa kiungo mkongwe nchini, Jonas Mkude, juu ya kuagwa kwa heshima zote baada ya kuitumikia Klabu ya Simba kwa miaka 13.

Alikuwa amebaki kuwa mchezaji pekee aliyesalia kwenye kikosi cha tangu msimu wa 2010/11, huku klabu yake ikitamka kuwa itamfanyia heshima ya kumuaga siku ya Tamasha la Simba Day Agosti 6, mwaka huu.

Mara baada ya kutangaza kuachana naye na kutokuwa sehemu ya kikosi kwa msimu ujao, viongozi wa klabu hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu, Imani Kajula na Meneja Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, Ahmed Ally, kwa nyakati tofauti walisema watamuaga kwa heshima zote mchezaji huyo.

Wakadai wasingeweza kumuaga kwenye mechi za mwishoni mwa Ligi Kuu, bali wametenga siku maalum ambayo huwa wanafanya hivyo miaka yote na hata msimu uliopita kina Meddie Kagere na wenzake waliagwa kwenye kilele cha Simba Day.

Lakini zikazuka tetesi kuwa huenda Mkude angejiunga na Klabu ya Yanga, hapo ndipo minong'ono ikaanza iwapo angetua Jangwani ni kweli klabu yake ingekubali kumuaga kama ilivyopangwa.

Lisemwalo lipo, na kama halipo linakuja, Klabu ya Yanga ikatangaza kusajili Mkude kwa mkataba wa mwaka mmoja, na atakuwa sehemu ya kikosi kwa msimu ujao.

Mashabiki wengi wa soka wakajua sasa suala hilo halipo tena, wakidhani kuwa Klabu ya Simba isingeweza kukubaliana na jambo hilo la kumuaga mchezaji ambaye anakwenda kuichezea timu ambayo ni wapinzani wao wa jadi.

Kwa namna ya uanamichezo na 'fair play' kama ambavyo Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) linasisitiza, Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed aliibuka na kusema hata kama Mkude amejiunga na Yanga, lakini azma yao ipo pale pale kumuaga kwa heshima kwani ameitumikia klabu yao kwa muda mrefu tangu yupo kikosi cha pili hadi anapandishwa kikosi cha kwanza.

Ofisa Mtendaji Mkuu, Kajula naye akaja kusisitiza kuwa kujiunga kwake Yanga hakumwondolei sifa ya kuwa yeye ni gwiji kwenye klabu yao, heshima yake inabaki pale pale, na ikimpendeza mwenyewe aje kuagwa kwani kujiunga na Yanga ni sawa mtu yeyote ambaye amepata kazi sehemu nyingine na haimwondolei sifa ya kuagwa.

Cha ajabu na kushangaza, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, kwa maneno ambayo si ya uanamichezo, akasema kuwa hawako tayari kumuachia mchezaji wao kwenda kuagwa na Simba.

Kwa hali ya kawaida ilitegemewa kuwa Simba ndiyo wangekataa kwa sababu mchezaji amekwenda Yanga, lakini waliomchukua mchezaji ndio wanakataa.

"Labda watafute Mkude mwingine wamuage kama shida ni kuaga, lakini siyo huyu, ila kama wanaona ni lazima wafanye hivyo basi tunawaalika wao waje Siku ya Mwananchi ili wamuage," akasema Kamwe.

Yaani kama Simba wana hamu sana basi waende kwenye Kilele cha Siku ya Mwananchi kitachofanyika Jumamosi Ijayo kwenda kumuaga.

Binafsi, kama mwanamichezo nimesikitishwa na kauli hii kwani si ya uanamichezo kabisa na haina 'fair play' ndani yake. Sidhani kama kuna kitu chochote kibaya kumuacha Mkude kwenda kuagwa halafu akarejea tena kwenye klabu yake.

Vita hii ya klabu na klabu haitaziathiri klabu hizi bali mchezaji mwenyewe kwenye maisha yake baada ya soka.

Kuna wachezaji wa zamani ambao sitowataja hapa, wamezichezea klabu hizi kwa muda mrefu na kuzipa mataji, lakini walimaliza karia zao vibaya na mpaka sasa hawapati heshima yoyote kwenye klabu hizo.

Hata klabu zinapotakiwa kuwataja walioipatia heshima huwa hawatajwi na wala hawaitwi kuchezea timu za veterani na hata wanapokuwa makocha hawapewi ajira na hawaaminiki.

Nimshauri tu Mkude asiwe mmoja kati ya wachezaji hao kwa sababu ameishi muda mrefu Simba na hadi leo ana mashabiki wake, hivyo hatakiwi kuwapoteza au kuwasaliti kwani na wao watamsaliti moja kwa moja na atakuwa mpweke nje ya maisha yake ya soka kama wachezaji wengine.

HABARI KITAIFA

# Mume auawa akimwokoa mkewe shambulio la fisi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MKAZI wa Kijiji cha Chiwambo, Kata ya Lulindi, wilayani Masasi, mkoani Mtwara, Haika Mangeja (62), amefariki dunia baada ya kuvamiwa na fisi wakati akijaribu kumwokoa mke wake.

Wananchi wa kijiji hicho walifika eneo la tukio na kumkuta fisi huyo akiwa anakula mwili wa marehemu eneo la kichwani na kumuua kwa kutumia silaha za jadi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Maimuna Mbaya, alisema kuwa tukio hilo lilitokea juzi saa saba usiku wakati Mangeja na mke wake, Asina Nguriko (49), wakiwa ndani ya nyumba yao wakiota moto na fisi huyo kuwashambulia.

Alisema Mangeja alifariki dunia wakati akimwokoa mke wake ambaye alikuwa akipambana na fisi huyo aliyefika katika nyumba yao.

Alisema wakati Asina akimfukuza fisi kwa kutumia mti, alimrukia na kumshambulia na kumjeruhi na ndipo mume wake alipokwenda kumwokoa na kupoteza maisha.

"Majeruhi ni wawili ambao ni Asina ambaye wakati mume wake akimwokoa mikononi mwa fisi, alifanikiwa kukimbia. Mwingine aliyejeruhiwa ni Rashidi Yusuph (72) ambao wote walikimbizwa katika Kituo cha Afya cha Nagaga kwa ajili ya matibabu," alisema.

Mbaya aliiomba mamlaka husika ifike katika kijiji hicho kwa ajili ya kuwaondoa wanyama hao ili wasiendelee kuleta madhara kwa wanakijiji.

Juma Bakari na Saidi Mtipa ambao ni miongoni mwa wanakijiji waliomuua fisi huyo, walisema walisikia sauti za watu wakiomba msaada na walipofuatilia walimkuta fisi huyo akila kichwa cha marehemu na ndipo walipomuua.

## Waziri aona fursa bima sekta ya nishati

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI wa Nishati ameizitaka kampuni za bima nchini kutumia fursa zilizoko katika Sekta ya Nishati, kuzitambua na kufahamu zina nafasi ya kuzifikia na kuzipata.

January Makamba alitoa rai hiyo juzi wakati wa ufunguzi wa semina ya kujadili ushiriki wa kampuni za bima nchini katika miradi ya nishati iliyofanyika jijini Arusha.

Waziri huyo alitoa wito kwa kampuni za bima na wadau wengine kufahamu kuwa milango iko wazi wizarani kuendelea kushirikiana nao na kuwasiliana kwa karibu.

Alisema wako tayari kuwapa ujuzi na maarifa ya mahitaji mahsusi ya Sekta ya Nishati ikiwamo upanuzi wa mtaji kutokana na ukubwa wa uwekezaji katika sekta hiyo.

Akizungumzia madhumuni ya mkutano huo, Waziri January alisema umelenga kujadiliana kwa kuwa kampuni za bima zimetengeneza umoja ambao unataka kujishughulisha na fursa zilizoko katika Sekta ya Nishati hasa miradi ya gesi na mafuta, miradi ya umeme na mingineyo katika Sekta ya Nishati.

"Kama mnavyofahamu, tunaelekea katika utekelezaji wa miradi mikubwa sana ya kimkakati ya nishati ikiwamo Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani (Tanga).

"Pia tuna mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia kule Lindi. Moja ya fursa zilizopo katika miradi hiyo mikubwa ya kimkakati ya nishati ni bima," alisema waziri huyo. Alifafanua zaidi kuwa bima ni sehemu ya huduma za fedha. Ni biashara kubwa. Kuna kampuni 22 ambazo zimetengeneza umoja wake nchini na zimeialika Wizara ya Nishati ili kufanya mazungumzo nao kueleza ni fursa zipi zilizopo za bima katika miradi ya nishati na wanaweza kuzifikia vipi fursa hizo, ushirikiano ambao unaweza kuwapo kati ya serikali, Wizara ya Nishati, taasisi na kampuni hizo.

Alisema mazungumzo ya kutekeleza Mradi wa Kusindika na Kuchakata Gesi kule Lindi yamemalizika na kukuwa mazungumzo na vipengele vinavyohusu bima.

Waziri huyo alisema mradi huo ni fursa kubwa. Thamani yake ni takribani Sh. trillioni 97. Lazima ukatiwe bima kubwa, hivyo kampuni hizo 22 zimejenga umoja ili kuhakikisha fursa hiyo zinaitumia na kuifikia.

January alisema kuwa nchini, ni Watanzania wachache wanaotumia bima na mwamko wa matumizi ya bima nchini bado mdogo.

Hivyo, alisema ni matumaini yake kuwa mkutano huu ulioandaliwa na Mamlaka ya Bima nchini (TIRA) pamoja na kampuni za bima utakuwa chachu katika kukuza tasnia ya bima nchini.

Akifafanua kuhusu ushiriki wa wazawa katika bima za miradi ya nishati wakati wa semina hiyo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Athumani Mbuttuka, alisema ni nia ya serikali kuhakikisha kampuni za bima nchini zinashiriki kikamilifu katika miradi ya nishati.

Kamishna wa TIRA, Dk. Baghayo Saqware, alisema lengo la kuunda konsotia (ushirika wa kampuni za bima) ni kutokana na ukweli kuwa miradi ya nishati inahitaji mitaji mikubwa na pia ni miradi ambayo vihatarishi vyake au majanga viko juu sana.

Alisema kampuni moja moja inaweza kupata changamoto katika kumudu kukinga majanga yanayoweza kutokea katika miradi hivyo, na hivyo kupelekea muungano huo.

Dk. Baghayo Saqware alitaja Kampuni Kiongozi ni Phoenix Insurance Company ambayo imeweka hisa kubwa katika konsotia hiyo. Itahusika na utafutaji wa masoko na kupokea sehemu ya majanga ambayo konsotia haitaweza kuyamudu.

Dk. Saqware alisema konsotia hiyo ilizinduliwa tarehe 16 Novemba 2022 na Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Chande.


MWANGA HAKIKABANK

MWANGA HAKIKA BANK LIMITED
MINIMUM DICLOSURE OF CHARGES AND TARIFFS

| PRODUCTS/ SERVICES | BUSINESS CURRENT A/C | PREMIUM CURRENT A/C | PERSONAL SAVING A/C | SALARY A/C | MTOTO SAVING A/C | JIPANGE SAVING A/C | WEKEZA GROUP A/C | MALENGO SAVING A/C | FOREX ACCOUNT USD & EURO | JIWEKEE SAVING A/C | MHB PAMOJA A/C | MSOMI ACCOUNT |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Account opening | 100,000.00 | 50,000.00 | 20,000.00 | 0 | 10,000.00 | 10,000.00 | 20,000.00 | 100,000.00 | 10 | 0 | 50,000.00 | 10,000.00 |
| Minimum operating Balance | 100,000.00 | 50,000.00 | 10,000.00 | 5,000.00 | 5,000.00 | 0 | 10,000.00 | 100,000.00 | 10 | 10,000.00 | 50,000.00 | 5,000.00 |
| Interest Payable | N/A | N/A | 3.00% | 3.00% | 6.00% | 2.00% | 3.00% | 2% < 10Mil, 4%>=10Mil | 0.50% | 2.00% | 2% | 3.00% |
| Interest bearing amount | N/A | N/A | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 50,000.00 | 100,000.00 | 5,000.00 | 20,000.00 | 500,000.00 | 20,000.00 |
| Monthly Mantainance fee | 20,000.00 | 10,000.00 | 2,500.00 | 2,500.00 | Free | Free | Free | Free | 2 | Free | Free | Free |
| Deposit | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Monthly Statement | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free | Free |
| Adhock statement Per page | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 | 1 | 2,000.00 | 2,000.00 | 2,000.00 |

OTHER CHARGES

| SERVICES | AMOUNT ( TZS) |
|---|---|
| Certificate of Balance | 30,000.00 |
| Confirmation to the Auditors | 30,000.00 |
| Search for information above 5 years | 15,000.00 |
| Cheque book cost (Per Leaf) | 600.00 |
| Status report | 30,000.00 |
| Stop payment order | 30,000.00 |
| Dishonoured cheque for lack of funds or refer to drawer or effect not cleared | 100,000.00 |
| Dishonoured cheque due to the technical error caused by customer | 60,000.00 |
| Dormant Account Activation | Free |
| Account Closing on Customer Demand | 10,000.00 |
| Counter cheque per leaf [Within the Bank] | 15,000.00 |
| Salary Processing fee [ per Transaction] | 1,000.00 |
| Customer ID | 10,000.00 |
| Pre-Mature breaking of Fixed Deposit on customer request | Minimum of 50% of the accrued interest |
| CCTV Camera footage searching request from Customer | 30,000.00 |
| Uncollected Cheque Book/Destruction | 5,000.00 |
| Visa Card Issuance-Classic | 10,000.00 |
| Visa Card Issuance-Gold | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Classic | 15,000.00 |
| Replacement Visa Card-Gold | 25,000.00 |
| Umoja Card Mantainance fee | 1000 per month |
| Visa Card- Classic Mantainance fee | 3,000 per QTR |
| Visa Card-Gold Mantainance fee | 5,000 per QTR |
| Uncollected ATM Card | 5,000.00 |
| PIN reset fee | 5,000.00 |
| Withdraw fee local (Umoja ATM) | 1000-99,000=1500 100,000-400,000=1700 |
| Withdraw fee other Bank (Domestic Banks) | 3,500 |
| Withdraw fee other Bank (International) | 11,000 |
| Balance inquiry Umoja ATM | 300 |
| Balance inquiry other Domestic Banks | 950 |
| Balance inquiry other Bank (International) | 2,000 |
| Decline Domestic [Insufficient fund] | 1,000 |
| Decline International [Insufficient Balance] | 1,500 |
| QR transactions | 3% of Transaction Amt |
| POS transactions | 3% of Transaction Amt |
| E-commerce transactions | 3% of Transaction Amt |

Cash Withdraw Over the Counter [TZS/ USD/EURO]

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Wekeza/Jiwekezee | 2,000.00 |
| Bellow 10 Mil | 3,000.00 |
| Above 10Mill to 50 Mil | 0.10% |
| Above 50Mil t0 100 Mil | 0.090% |
| Above 100Mil to 300 Mil | 0.089% |
| Above 300 Mil | 0.079% |

Cash Withdraw Over the CounterForeign Currency [USD/EURO]

| TRANSACTION AMOUNT | RATES |
|---|---|
| Below USD/EURO 4,000 | 2 |
| Above USD/EURO 4000 | 0.1% more than USD/EURO 40 |

AGENCY BANKING CHARGES

| TYPE OF SERVICES | RATES |
|---|---|
| Deposit | Free |
| Balance Inquiry | 500 |
| Min Statement | 700 |
| Transfer of fund within MHB | 2,000 |
| Transfer of funds to other Bank | 13,000 |

AGENCY BANKING WITHDRAWAL FEE

| AMOUNT | FEE |
|---|---|
| Up to 50,000 | 850.00 |
| 50,000 - 100,000 | 1,000.00 |
| 100,000 - 300,000 | 2,000.00 |
| 300,000 - 500,000 | 3,500.00 |
| 500,000 - 1,000,000 | 4,500.00 |
| 1,000,000 - 3,000,000 | 6,000.00 |
| 3,000,000 - 5,000,000 | 10,000.00 |

MOBILE BANKING CHARGES

WITHDRAWAL CHARGES

| MINIMUM [TZS] | MAXIMUM [TZS] | RATES [TZS] |
|---|---|---|
| 0 | 10,000 | 800 |
| 10,001 | 19,999 | 1,800 |
| 20,000 | 49,999 | 3,500 |
| 50,000 | 99,999 | 5,200 |
| 100,000 | 199,999 | 7,200 |
| 200,000 | 499,999 | 8,200 |
| 500,000 | 999,999 | 10,500 |
| 1,000,000 | 2,000,000 | 11,200 |
| 2,000,001 | 3,000,000 | 12,000 |
| 3,000,001 | 5,000,000 | 15,000 |

FUND TRANSFER CHARGES

| | |
|---|---|
| Transfer of Funds within MHB | 2,000.00 |
| Transfer of funds to other Banks | 13,000.00 |

EFT/SWIFT/TISS

| | |
|---|---|
| EFT within the Bank (Incoming) | Free |
| EFT to other Banks | 1,500.00 |
| TISS Transfer | 10,000.00 |
| T.T. Transfer | - |

STANDING ORDER

| | |
|---|---|
| Instructions within MHB | FREE |
| Standing Order to other Bank | 10,000/= |

www.mhbbank.co.tz

# Nyumba yabomolewa bila kibali

**Na Gwamaka Alipipi**

WATU wasiofahamika wanaodaiwa kutokuwa na kibali, wamevunja nyumba na kupora mali za mkazi wa Ununio, Dar es Salaam, Paul Mbwana. Tukio linalodaiwa kufanywa Juni 21, mwaka huu saa 12 jioni.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Mbwana alisema watu hao walifika katika nyumba yake iliyoko Ununio na kuvunja nyumba kisha kuondoka na baadhi ya vitu vya ndani ikiwamo televisheni, laptop na madirisha.

Alisema alinunua eneo hilo mwaka 2000 na akaanza mchakato wa kupata hatimiliki mwaka 2008, kisha kujenga nyumba mbili katika eneo hilo.

"Kwa sasa siko Dar es Salaam lakini kuna ndugu zangu wanakaa huko. Siku ya tukio nimeambiwa walikuja vijana sita waliobeba vifaa vya kubomoa na kuanza kubomoa kisha kuchukua baadhi ya vitu vya ndani," alisema.

Mbwana alisema kuwa baada ya kutokea tukio hilo, alitoa taarifa kituo cha polisi na kuandikiwa WMB/RB/605/2023, ikieleza ni wizi wa vitu vya ndani, lakini hadi leo hakuna mtuhumiwa yoyote aliyekamatwa.

Akizungumza kuhusu tukio hilo, mtoto wa Mbwana, Collin Mbwana alisema: "Siku hiyo nilikuwa nimetoka nyumbani majira ya jioni, wakati narudi nikakuta nyumba imebomolewa na baadhi vya vitu havipo".

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Ununio, Mwinjuma Mwinyihija Shehe, alisema anafahamu kiasi kuhusu mgogoro uliopo kwenye eneo hilo.

Alisema siku ya tukio walikuja watu ofisini kwake wakitoa taarifa ya kwenda kuvunja nyumba, lakini alipowaomba kibali hawakuwa nacho. "Sisi haturuhusu mtu kuvunja pasi na kibali. Hivyo, sikuwapokea na wakaondoka wakasema wanakwenda kutafuta kibali. Sasa siku ya tukio walinipigia simu wakisema wanakuja kuvuja na wanataka usimamizi lakini hawakurudi tena kwangu. Ninachoweza kusema wamevunja nje ya utaratibu," alisema.

Mmoja wa majirani wa eneo hilo, John Alex, alisema: "Wiki moja iliyopita nilisikia kishindo. Nikatoka nje kujua kuna nini, nikawaona vijana wakiwa wamebeba nyundo wanavunja nyumba, nikawauliza wakasema wana kibali." Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Mtatiro Kitinkwi, alimtaka Mbwana kwenda kituo cha polisi alipofungua kesi na kumwuliza mpelelezi wa jadala la kesi yake linavyoendelea.

Alisema: "Ni haki yake kufahamu hatua ya kesi yake ilipofikia, asilalamike kwamba haijafanyiwa kazi. Jeshi la Polisi kazi yake ni kuzuia uhalifu na kuwakamata wahalifu. Sitaki kuamini kama hao watu wanalijulikana na hawajakamatwa."




Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kidigitali wa Bank of Africa Tanzania, Jesse Jackson (kulia), akimkabidhi zawadi ya simu janja Jesca Alex Rutta, ambaye ni mshindi wa droo ya tatu ya kampeni ya benki hiyo, huduma za kidigitali ya 'Fanya Mhamala Ushinde', Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madereva watakiwa kuwa 'macho' ulinzi wa watoto

**Na Halfani Chusi**

MADEREVA wa magari ya shule na walezi wa wanafunzi wametakiwa kuwa walinzi namba moja wa mtoto kwa kufuatilia nyendo zao, ili kubaini mapema kama wanafanyiwa vitendo vya ukatili na kuwaepusha kuingia katika matatizo.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, wakati akifungua mafunzo maalum ya kuwajengea uwezo madereva wa magari ya shule na walezi wa wanafunzi katika shule mbalimbali za wilayani humo yaliyoandaliwa na Taasisi ya Mpango wa Usalama Barabarani (TARSI).

Mtambule alisema madereva na walezi hao ndio wanakaa muda mwingi na watoto kuliko wazazi, hivyo ni rahisi kugundua kama mtoto ana tatizo kwa kumwangalia namna atakavyokuwa anashirikiana na wenzake kipindi chote anapokuwa shuleni au katika gari wakati wa kumchukua na kumrudisha.

"Mtoto mara nyingi utasikia amebakwa na mzazi wake wa kumzaa, amebakwa na mjomba wake. Ukimpeleka shuleni utasikia nako amebakwa na mwalimu wake, katika nyumba za ibada nako hivyo hivyo. Sasa wakati mwingine unajiuliza hawa watoto wetu wapi watakuwa salama?

"Serikali haitamvumilia mtu yeyote atakayebainika na kosa la kumfanyia mtoto ukatili, tutachukua hatua kali dhidi yake, ili iwe fundisho kwa wengine," alionya kiongozi huyo.

Pia aliwataka wananchi kutoa taarifa mapema pale wanapoona ukatili umefanyika na kushiriki mahakamani kutoa ushahidi pale wanapohitajika, ili mhalifu wa vitendo hicho apatiwe adhabu anayostahili kwa mujibu wa sheria.

Aliipongeza Taasisi ya TARSI kwa kuandaa mafunzo hayo huku akiwataka madereva na walezi wayatumie katika maeneo yao ya kazi ili kuleta tija.

Mkurugenzi wa TARSI, Maliki Barongo, alisema lengo la kuja na programu hiyo ni kuwajengea uwezo madereva na walezi katika suala la malezi na usalama barabarani, akisisitiza kuwa lengo lao ni kuifika nchi nzima.

Alisema mafunzo hayo yatasaidia madereva hao kupunguza ajali za barabarani pamoja na ukatili wa kijinsia na hatimaye watoto kuwa salama na kutimiza ndoto zao.

Aliwaomba wadau wengine wajitokeze kuiunga mkono taasisi yao, ili kuwezesha kuifikisha elimu ya usalama barabarani nchi nzima.

Mkuu wa Dawati la Elimu ya Usalama Barabarani wa Kikosi cha Usalama Barabarani (makao makuu), Michael Deleli, alisema mafunzo hayo yataongeza ufanisi kwa madereva wa magari ya shule na kuwa chachu ya kupunguza ajali za barabarani.

Mmoja wa madereva waliohudhuria mafunzo hayo, Salum Mayanda kutoka Shule ya Green Acre, aliishukuru taasisi hiyo kwa kuwapa mafunzo pamoja na serikali kuamua kila basi la shule kuwa na walezi wanawake kwa kuwa walijikuta wakati mwingine wakisingiziwa vitendo ambavyo hawajavifanya.

Mlezi kutoka Shule ya Feza, Malina Mboma, alisema kutokana na kukithiri vitendo vya ukatili wa kingono, wamekuwa makini na watoto wanapopanda mabasi ya shule ikiwamo kuwazuia kupakatana.

# Serikali yafuatilia wenye sifa kuingizwa miradi ya TASAF

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amesema serikali inaendelea kufuatilia wenye vigezo vya kuingizwa katika mpango wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili wanufaike na miradi.

Ridhiwani pia ameelekeza TASAF kuhakikisha tathmini ya wanufaika wa kaya maskini haiwaondoi watu katika mpango kwa kuwa wana nyumba na badala yake kupatikana kwao na kuondolewa kutokane na mikutano ya vijiji.

Naibu Waziri huyo alielekeza hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na wanufaika wa TASAF katika Wilaya ya Bagamoyo, wengi wao wakiwa wamejikita katika ujasiriamali baada ya kunufaika na fedha zinazotolewa na mfuko huo kwa misimu tofauti.

"Msiwaondoe watu katika mpango kwa kigezo cha nyumba ya kuishi. Hiyo siyo alama ya utajiri na wengine wanapenda kuvaa vizuri lakini hali zao za maisha bado ni duni," Ridhiwani alitoa angalizo.

Alisema kuwa katika mwaka wa fedha 2022/23 na 2023/24, seikali imetenga jumla ya Sh. bilioni 51 kwa ajili ya miradi mbalimbali inayotekelezwa na TASAF kwa kaya maskini.

Mwanahawa Hassan, mkazi wa Bagamoyo, ni miongoni mwa wanufaika wa mpango wa kusaidia kaya maskini wa TASAF ambaye tayari amejikita katika shughuli za ujasiriamali na kuwa na mabadiliko katika maisha yake.

Mwanahawa alisema tayari amenufaika na mkopo wa Sh. milioni saba ambao umemwezesha kuinua biashara zake, jambo ambalo limemfanya kuomba kuondolewa katika mpango kwa kukosa vigezo vya kuendelea kubaki.

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Pwani, Roselyn Kimaro, alisema Wilaya za Kibaha, Kisarawe na Bagamoyo ni miongoni mwa maeneo yenye wanufaika wa kaya maskini ambao baada ya kuingizwa katika mpango wa TASAF wamekuwa na mabadiliko ya makazi na maisha kwa ujumla.

Kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia ya Mwaka 2020, Tanzania ni miongoni mwa mataifa yanayokabiliwa na umaskini. Kina cha umaskini kikiwa asilimia 26.4.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka jana, umaskini wa mahitaji ya msingi ni mkubwa kwa maeneo ya vijijini kwa asilimia 31.3 kulinganishwa na maeneo ya mijini ambayo ni asilimia 15.8.

Awamu ya tatu ya mradi wa TASAF ilizinduliwa mwaka 2020 ukiwa na thamani ya Sh. trilioni mbili zinazotumika kutoa ruzuku kwa kaya maskini na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za elimu, afya na miundombinu.



## HABARI KANDA KASKAZINI

# TPC yagawa matrekta kwa wakulima wa mpunga

**Na Godfrey Mushi,**
SIMANJIRO

KIWANDA cha Sukari cha TPC kupitia Shirika lake la FTK, limewapatia matrekta madogo mawili maarufu 'power tiller' wakulima wa Kijiji cha Kiruani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara ili waweze kuchavanga mashamba yao ya mpunga.

Matrekta hayo yana thamani ya zaidi ya Sh.milioni 18.34, kwamba yatawasaidia wakulima hao katika uzalishaji wa zao hilo.

Kwa miaka mingi, wakulima hao ambao ni wanachama wa Chama cha Wakulima wa Mpunga Kiruani (CHAMPIKI), wamekuwa wakisotea huduma hiyo ya matrekta madogo ya kilimo, kwa kukodi vijiji vya jirani, jambo ambalo limeathiri uchumi wao.

Akizungumza jana wilayani humo na wakulima hao, wakati wa hafla ya makabidhiano ya matrekta hayo na darasa la awali la Shule ya Msingi Kiruani, Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPC, Japhary Alli, alisema wameamua kuwawezesha wakulima hao wakiamini yatawasaidia kujikwamua kiuchumi na kufikia malengo yao ya uzalishaji wa chakula.

Ujenzi wa darasa hilo la awali, umeigharimu TPC/FTK Sh. milioni 44.8 ukijumuisha ujenzi wa darasa pamoja na ofisi ya mwalimu, meza, viti, makabati na uchoraji wa picha ukutani kwa ajili ya kufundshia watoto.

Kabla ya makabidhiano hayo, Meneja wa FTK, Nina Sharif, alisema awali wakulima wa Kiruani walikuwa wakitumia pesa nyingi kukodisha matrekta kutoka vijiji jirani na kwa uchache wa vifaa hivyo, baadhi ya wakulima hupitwa na muda ambao wangepaswa kuwa tayari wamesha chavanga mashamba yao kwa ajili ya msimu wa kupanda.

"Uhitaji bado ni mkubwa, hivyo basi kamati teule ya usimamizi itapanga mkakati wa ufanyaji kazi wa power tiller hizi ili ziweze kuzalisha fedha na kununua power tiller nyingine.

"Ni matarajio yetu kwamba power tiller hizi zitatumika kuleta maendeleo na mapato yatakayopatikana yatatumika kufanya matengenezo ya power tiller, wakati itakapohitajika."

Mwenyekiti wa Chama cha Umwagiliaji Kiruani (CHAWAKI), Izack Leseyo, akieleza matarajio yao baada ya kupata matrekta hayo alisema: "Kijiji cha Kiruani kilianzishwa mwaka 1975 na mpaka kufikia sasa tunalo eneo la mashamba ya kilimo cha umwagiliaji hekta 5,000, eneo sasa hivi tunalolima mpunga ni ekari 200, eneo lingine linalimwa mahindi, mboga na maharage.

"Ujio wa hizi power tillers, ambazo tumeletewa na FTK, baada ya sisi kuwaomba watusaidie na wakatupa mafunzo kuhusu umwagiliaji, utatusaidia sana kuongeza eneo la uzalishaji wa mpunga kutoka ekari 200 za sasa hadi kufikia ekari 5000.5."

Diwani wa Kata ya Msitu wa Tembo, Kaleya Mollel, aliwashukuru TPC na FTK kwa misaada hiyo, akisema amekuwa akipeleka mahitaji kwao.

"Nimepeleka ombi la madawati ya sekondari, wamenikubalia kuna mambo wanaweka sawa na tutapata hayo madawati kwa ajili ya sekondari yetu," alidokeza kuhusu ombi hilo pia.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji, ambaye ni Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Happyness Masatu, akizungumza baada ya kupokea power tiller hizo, alionya matrekta hayo yasiwe chombo cha mtu mmoja kujimilikisha kwa manufaa yake.peke yake.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kushoto), akimkabidhi vifaa vya kutolea huduma za maji fundi wa vyombo vya watumia maji kutoka Wilaya ya Kiteto, Grace Msovela, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Kampuni ya Ubongo kuadhimisha miaka 10

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

KAMPUNI ya Ubongo inayoongoza kwa uzalishaji wa vipindi vya elimu burudani Afrika, imetangaza maadhimisho ya miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, huku ikijivunia kufikia familia zaidi ya milioni 30 Afrika na kuleta mabadiliko katika sekta ya elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Ubongo, Mwasi Wilmore alisema kupitia mkusanyiko wa programu za elimu zinazovutia ikiwamo akili and me, ubongo kids na nuzo and namia iliyoanzishwa hivi karibuni, kampuni hiyo imeendelea kuwa kinara katika nyanja ya ubunifu katika ujifunzaji wa watoto.

"Tangu kuanzishwa kwake Julai 2013 jijini Dar es Salaam, nchini Tanzania, Kampuni ya Uongo imejikita katika kutengeneza maudhui ya elimu yenye kufurahisha, kuelimisha na yenye kuzingatia lugha na tamaduni za kiafrika zinazomfanya mtoto apende kujifunza.

"Kupitia teknolojia mbalimbali kama vile televisheni, redio, na simu za mkononi, Kampuni ya Ubongo imeweza kufikia familia zaidi ya milioni 32 Afrika na kufanya athari kubwa katika sekta ya elimu ya bara hili," alisema Mwasi.

Aliongeza kuwa utafiti huru zilizochunguza programu za ubongo zimeonesha mara kwa mara matokeo mazuri kama vile kuboresha utayari wa mtoto kuanza shule na viwango vya ujifunzaji, kuchangia mabadiliko chanya ya kijamii na kitabia kwa watoto na walezi wao.

Alisisitiza kuwa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, ubongo imekua kutoka shirika dogo la Tanzania hadi shirika lisilo la kiserikali lenye uwakilishi wa kina barani Afrika na kuwa kinara katika elimu-burudani barani Afrika.

Mwasi alisema kuwa programu za ubongo zilizojaa ubunifu na zenye kusisimua, zinawawezesha watoto kupata maarifa na stadi muhimu zinazowasaidia kubadili maisha yao na jamii zao kwa ujumla.

# ONG yatoa zawadi kwa wasichana wabunifu Arusha

**Na Getrude Mpezya,** ARUSHA

SHIRIKA la kiraia la Okoa New Generation (ONG), linaloendesha mradi wa kusaidia wasichana, vijana na jamii ya watu wenye walemavu (EPIC), limekabidhi hundi ya Sh. 500,000 kwa wasichana wajasiriamali wabunifu wa Jiji la Arusha, baada ya kufanya vizuri katika maonyesho ya biashara.

Kwa mujibu wa Mratibu wa shirika hilo na mwandaaji wa mashindano ya ubunifu, Shaban James, alisema kuwa utoaji wa motisha ni hamasa kwa mabinti wengine wanaojishughulisha na ujasiriamali kujiepusha kuendelea kuwa tegemezi.


Alisema 'Okoa' wanatumika kushawishi mabinti kwa kufanya mafunzo ya biashara na ujasiriamali ili kuwasaidia kuanzisha na kumiliki biashara pamoja na kufundishwa vyanzo vya upatikanaji wa mitaji ama kuwapatia mitaji ili kufanikisha biashara zao kuwa endelevu.

"Malezi na ushauri humsaidia na kumwongoza binti mbunifu kwa kila hatua katika biashara yake na jinsi ya kufanya biashara kidigitali ili kuwafikia wateja kwakuwaunganisha na wafanyabiashara," alisema James.

Ofisa Maendeleo ya Vijana, Japhet Kurwa, alisema kuwa utoaji wa elimu na misaada kwa wajasiriamali wadogo ni lazima kijana apate elimu na kuwa na utayari wa kuchangamkia baadhi ya fursa za biashara zinazojitokeza ili kutimiza ndoto zao na kumsaidia kijana tunatakiwa kuwaandaa vijana vizuri na kuanza kuwekeza katika kutumika," alisema.

Hata hivyo moja ya mshindi na mwelimishaji rika, Piala Silayo, alisema kuwa yeye kama mnufaika wa shirika hili anawashauri mabinti wenzake kuwajasiriamali ili kuepuka kutegemea kipato kutoka kwa wanaume na kupelekea maambukizi ya magonjwa ya zinaa na badala yake wapambane wawe wafanyabiashara wenye ubunifu.

Naye Naibu Meneja mradi wa asasi inayosaidia mabinti, vijana walioko nje ya shule na wanaoishi na maambukizi ya Virusi Vya UKimwi (SHDEPHA), Irene Jacob, alisema wataendelea kufanya kazi kwa ajili ya kuwasaidia vijana hawa ili kufikia malengo na kupata Taifa lenye wajasiriamali na wafanyabiashara wenye kutimiza ndoto zao.





# Serikali yatoa ufafanuzi kero tano sekta ya afya Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI imetoa ufafanuzi na utatuzi wa kero tano zinazoikabili sekta ya afya mkoani Shinyanga ambazo ni ukosefu wa jengo la kuhifadhia maiti, uhaba wa madaktari bingwa, ukosefu wa magari ya wagonjwa, uhaba wa majengo, wahudumu wa afya.

Kero hizo zilizoibuliwa wakati wa ziara ya siku mbili ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu mkoani hapa, kwamba wakazi walieleza kuwa kero hizo zimekuwa zikiwagharimu pindi wanapofika katika vituo vya afya, hospitali kupata matibabu.

Akijibu kero ya ukosefu wa jengo la kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Rufani Mkoa, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndugile alisema licha ya hospitali hiyo kuanza kutoa huduma za matibabu Novemba mwaka jana bado ina matatizo kadhaa yanayokwamisha baadhi ya utendaji kazi.

Alitaja mapungufu mengine kuwa ni pamoja na uhaba wa magari ya kubebea wagonjwa kwamba uhitaji ni magari 45, lakini kwa sasa yapo 13.

"Tuna madaktari bingwa wawili wa magonjwa ya watoto, magonjwa ya ndani mmoja, upasuaji mmoja na magonjwa ya kinamama mmoja, hivyo idadi hii ni ndogo kulingana na uhitaji wa hospitali hii," alisema Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga, Dk. Luzila John.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, akisoma taarifa ya huduma za afya wilayani humo, alisema wanakabiliwa na tatizo upungufu wa watumishi wa afya 874, kwa sasa waliopo ni 318 na uhitaji ni watumishi 1,192.

Alisema wilaya hiyo ina hospitali mbili, moja Serikali na nyingine ya binafsi, vituo vya afya 64, na zahanati 51 na pia inakabiliwa na upungufu wa majengo ya huduma mbalimbali zikiwamo huduma ya mama na mtoto.

Akijibu kero hizo Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alieleza kuwa serikali itahakikisha wanaongeza majengo katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga likiwamo jengo la monchwari pamoja na hospitali nyingine zenye uhitaji.

Kuhusu upungufu wa madaktari bingwa alisema tatizo hilo ni la nchi nzima na kwamba serikali ilitoa maombi ya ajira kwa madaktari bingwa 35, lakini walioomba 15 waliokidhi vigezo 11 na walioripoti kazini walikuwa sita tu.

Alisema serikali imeshatafuta njia ya mbadala ya kuwafanya madaktari bingwa wabaki kwenye hospitali za serikali na kutokimbilia hospitali binafsi.

Kadhalika, alitaja tatizo la uhaba wa watumishi wa afya kuwa lipo maeneo mengi nchini, kwani kama wizara haikuwa na kibali cha kuajiri kutoka kwa Rais, kwamba mwaka huu ndiyo wamepewa kibali na kuagiza halmashauri zitenge mapato ya ndani kuajiri watumishi wa afya kwa mkataba.

Kuhusu magari ya kubebea wagonjwa, Waziri Ummy alisema serikali itatoa magari kudhibiti adha hiyo na kusema kuwa kwa hatua ya awali watatoa magari matatu, mawili kutoka TAMISEMI na moja kutoka Wizara ya Afya ili kupunguza makali ya kero hiyo.

## Chato kuunganishwa katika mradi wa BBT

**Na Daniel Limbe,** CHATO

SERIKALI imesema ipo tayari kuiunganisha Wilaya ya Chato iliyopo mkoani Geita katika mradi wa BBT kutokana na wilaya hiyo kuonesha kuwa tayari ipo kimkakati katika kuinua uchumi kupitia kilimo cha umwagiliaji.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya mapinduzi ya kilimo na uchumi wilayani humo na kuipongeza wilaya hiyo kuwa ya kwanza kitaifa kutekeleza mwongozo wa kilimo.

Aidha, alisema wilaya hiyo itapewa kipaumbele cha utekelezaji wa miradi ya uchimbaji mabwawa ya umwagiliaji, upatikanaji haraka wa mbolea za viwandani kuanzia msimu wa kilimo 2023/24, mbegu bora na ushauri wa ugani kwa wakulima wote kwa lengo la kuhakikisha wanaufaika na kilimo biashara.

Alieleza kuwa hatua hiyo inalenga kupunguza kadhia ya ukosefu wa ajira kwa vijana na wanawake, kwamba kupitia mradi huo wananchi watakuwa na matumaini mapya ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mkuu wa Wilaya ya Chato, Mhandisi Deusdedith Katwale, alisema hali ya umaskini kwa wananchi katika wilaya hiyo imekuwa ikimsikitisha licha ya wilaya hiyo kuwa na rasilimali kubwa ya ardhi inayoweza kuwaondolea umaskini wa vipato.

Alisema kupitia ofisi yake waliamua kutumia wataalamu kutoka Chuo cha Kilimo cha Sokoine (SUA) waliosaidia kuandaa mkakati thabiti wa kufikia lengo la serikali la kuhakikisha wananchi wananufaika na kilimo biashara na kuachana na kile cha mazoea ambacho hakina tija.

Mtaalamu wa mifumo ya umwagiliaji kutoka SUA, Mhandisi Jackson Masakia, aliomba serikali kuwapatia sehemu ya ardhi kwenye wilaya hiyo ambayo watalima na kuzalisha kwa tija ili kuwaonyesha wananchi kwa vitendo kuwa kilimo biashara kinawezekana na ndiyo mkombozi mkuu wa uchumi wa kaya na taifa kwa ujumla.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Butata, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakiwa katika maktaba ya shule kwa ajili ya kujisomea mwishoni mwa wiki. Maktaba hiyo imejengwa kwa nguvu za wananchi, mbunge na Shirika la Kimataifa la Project Concern International (PCI). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC ahimiza wananchi kushiriki shughuli za maendeleo

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MKUU wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, amewataka wananchi wilayani humo kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika shughuli za kimaendeleo.

Alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki ofisini kwake wakati akielezea ujio wa Mwenge wa Uhuru wilayani humo, huku akiwataka wananchi kujitokeza kwa wingi siku ya kuupokea na kushiriki katika miradi itakayozinduliwa.

Alisema lengo la Mwenge wa Uhuru kufika wilayani hapa ni kuitambua miradi hiyo na kuitumia vyema pale inapoanza kutoa huduma.

Ngaga alisema Mwenge wa Uhuru utakuwa wilayani humo kwa siku mbili kutokana na wilaya hiyo kuwa na halmashauri mbili ambapo Julai 16 umepokelewa katika Halmashauri ya Buchosa Kijiji cha Isenyi na Julai 17 utakimbizwa katika Halmashauri ya Sengerema.

Alitaja miradi ya maendeleo itakayokaguliwa na Mwenge wa Uhuru ni 15 ikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. bilioni nane, ikijumuisha miundombinu ya barabara, miradi ya elimu, maji na afya katika Halmashauri ya Buchosa na Sengerema.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi wilayani humo waliahidi kutumia vyema fursa ya Mwenge wa Uhuru ikiwa ni pamoja na kushiriki katika shughuli za kibiashara wakati siku zote.

Walisema Mwenge wa Uhuru unahamasisha watu kufanya kazi kwa bidii, kwamba ukifika wilayani kwako watapata manufaa na miradi ambayo itazinduliwa.

Nipashe
# Spotika




NUKUU YA DECLAN RICE WA ARSENAL, UKURASA 13




# MAMBO MAWILI MBAPPE ANAWEZA KUIPA MADRID

**MADRID,** Hispania

KWA mujibu wa Fabrizio Romano, Paris Saint-Germain wamempa Kylian Mbappe muda wa kuamua juu ya mustakabali wake katika klabu hiyo, kwani mkataba wake katika timu hiyo utakamilika msimu ujao wa majira ya joto.

Taarifa za ziada pia zinaonesha kuwa uongozi wa klabu hiyo hauko tayari kumpoteza Mbappe bure msimu ujao wa majira ya joto. Kwa hiyo, ni ama atasaini nyongeza ya mkataba au uongozi utachunguza chaguo gumu, lakini muhimu la kumuuza msimu huu ujao.

Real Madrid ni moja ya klabu zilizo na uwezo mkubwa wa kifedha na wameonesha nia hadharani na pia wamekuwa na nia ya kumsajili Mfaransa huyo. Hakuna wasiwasi kwamba Mbappe anaweza kuonekana kama mbadala makini wa Karim Benzema.

Fowadi huyo mzaliwa wa Paris ni mmoja wa wachezaji wa kutumainiwa wa Paris Saint-Germain na uwezo wake wa kushambulia ni mkubwa zaidi. Zaidi ya hayo, uwezo wake wa kusaidia timu ni mkubwa na wa kusifiwa.

Kwa maelezo hayo, orodha hii inaangalia mambo mawili ambayo Mbappe anaweza kuwapa Real Madrid iwapo uhamisho wake utawezekana kutokea msimu huu wa majira ya joto, twende sasa...

**#2. Ubunifu na uwezo wa kushambulia**

Unapozungumzia washambuliaji mahiri barani Ulaya na kwingineko, mojawapo ya majina yanayokuja kichwani ni Mbappe kama umahiri wake wa kutengeneza nafasi kwenye nusu ya mpinzani. Hayo hapo juu yamethibitishwa vya kutosha kwani ametoa jumla ya asisti 98 katika mechi 260 akiwa fowadi wa Paris Saint-Germain.

Pili, katika suala la uimara wa kushambulia, Mbappe pia ni miongoni mwa wachezaji wanaoweza kucheza nafasi nyingi za ushambuliaji kwani anaweza kucheza namba tisa, saba na 11. Mfaransa huyo pia anaweza kuchukua nafasi ya mshambuliaji mwenzake pindi itakapohitajika.

**#1. Ataboresha kiwango cha ufungaji**

Karim Benzema ndiye mfungaji bora wa Real Madrid na mwenye heshima zaidi katika kipindi cha miaka minne iliyopita huku akiifungia klabu hiyo mabao mengi ya kushinda mechi. Hata hivyo, baada ya kuondoka kwake, mmoja wa wachezaji wanaoweza kuziba pengo la mshambuliaji huyo wa kati ni Mbappe.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa AS Monaco alifunga mabao 41 kwenye michezo 43 katika mashindano yote akiwa na Paris Saint-Germain msimu uliopita.

Zaidi ya hayo, alikuwa mfungaji bora wa Ligue 1 msimu wa 2022-23 akiwa na mabao 29, akimshinda Alexandre Lacazette, aliyefunga mabao 27 na alikuwa mpinzani wake wa karibu zaidi. Ameifungia klabu hiyo mabao 212 katika mechi 260.

Kwa kuzingatia namba zilizo hapo juu, pamoja na washambuliaji wa kiwango kama Vinicius Junior na Rodrygo katika safu ya ushambuliaji ya Real Madrid, hakuna shaka kwamba watatu hao wanaweza kusambaratisha safu kadhaa za ulinzi kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga na mashindano mengine ya Ulaya.

Inabakia kuonekana ikiwa Real Madrid itavunja benki na kumsajili Mfaransa huyo, ambaye kwa sasa thamani yake ni euro milioni 180 kwa mujibu wa takwimu za uhamisho.

## ISIKUPITE

HUU ndio usajili wa Klabu za 'Top 3' Ligi Kuu Bara hadi sasa kuelekea msimu wa 2023/24. Yanga: Nickson Kibabage (Tanzania), Gift Fred (Uganda), Jonas Mkude (Tanzania), Kouassi Attohoula Yao (Ivory Coast) na Maxi Mpia Nzengeli (DR Congo). Simba: Willy Essomba Onana (Cameroon), Aubin Kramo (Ivory Coast), Che Fondoh Malone (Cameroon), David Kameta 'Duchu' (Tanzania) na Fabrice Ngoma (DR Congo). Azam FC; Feisal Salum 'Fei Toto' (Tanzania), Djibril Sillah (Gambia), Alassane Diao (Senegal) na Cheikh Sidibe (Senegal).





MENDY

# KLABU 5 ZILIZOINGIZA FEDHA NDEFU KWENYE USAJILI HUU

**LONDON,** England

SOKO la uhamisho wa majira ya joto la 2023 kwa sasa linavuma huku mikataba mbalimbali ikikamilika na mazungumzo yanaendelea kati ya klabu kwa ajili ya wachezaji.

Klabu zote Ulaya zinaboresha na kuimarisha vikosi vyao kabla ya msimu mpya kuanza mwezi ujao.

Baadhi ya klabu bora barani Ulaya zimeonesha nia ya kweli sokoni kwa kutoa fedha ili kuleta wachezaji waliowalenga. Kadiri klabu inavyotumia, inafaa pia kusawazisha vitabu kwa kutengeneza faida kubwa.

Mapato yanayotokana na mauzo ya wachezaji huwezesha klabu kuzalisha fedha ambazo zinaweza kutumika kusajili wachezaji zaidi na pia kuwekeza katika maeneo mengine.

Pia husaidia kudhibiti vitabu kwa mujibu wa kanuni za kifedha za haki sawa (Financial Fair Play) ambazo zinasema kuwa klabu haipaswi kutumia zaidi ya inachozalisha.

Hivyo basi, makala haya yanaangalia klabu tano ambazo zimeingiza fedha nyingi hadi sasa katika kipindi hiki cha uhamisho wa wachezaji kinachoendelea...

**#5. Wolverhampton Wanderers - Euro Milioni 92.05**

Cha kufurahisha, Wolverhampton Wanderers ni moja ya klabu ambazo zimepata mapato mengi katika soko la sasa la uhamisho. Timu hiyo ya Ligi Kuu England imepata euro milioni 92.05 kutokana na mauzo ya wachezaji kufikia sasa.

Uuzaji wa Ruben Neves kwa Al Hilal ndio sababu kuu ya mapato haya mazuri. Kiungo huyo wa kati wa Ureno aliuzwa kwa klabu hiyo ya Saudia kwa dau la euro milioni 55. Wolves pia imewauza mabeki wa kati Conor Coady na Nathan Collins kwa Leicester City na Brentford kwa ada ya jumla ya euro milioni 35.55.

Zaidi ya hayo, kiungo wa Japan, Hayao Kawambe alihamishiwa Klabu ya Ubelgiji ya Standard Liege kwa euro milioni 1.50.

**#4. Sporting CP - Euro Milioni 108**

Miamba wa Ureno Sporting CP pia wamenufaika kwa wingi kutokana na mauzo ya wachezaji msimu huu wa majira ya joto. Wamepata euro milioni 108 kufikia sasa kutokana na mauzo ya wachezaji watatu.

Kiungo wa kati wa Uruguay, Manuel Ugarte, hivi majuzi alijiunga na Paris Saint Germain (PSG) kwa dau la pauni milioni 60. Mkataba huo unamfanya raia huyo wa Uruguay kuwa mchezaji ghali zaidi wa klabu hiyo kuuzwa nje ya nchi, ukimtoa Bruno Fernandes ambaye aliuzwa kwa Manchester United kwa euro milioni 55.

Sporting pia imepata euro milioni 40 kutokana na mauzo ya Pedro Porro kwenda Tottenham Hotspur msimu huu wa majira ya joto. Mshambuliaji Tiago Tomas pia alijiunga na VfL Wolfsburg kwa euro milioni nane.

**#3. Borussia Dortmund - Euro Milioni 108**

Borussia Dortmund wanasifika kwa kusaka vipaji vya vijana, kuwakuza katika ubora wa hali ya juu, na baadaye kuwauza kwa bei kubwa. Tangu msimu wa 2000-01, klabu hiyo ya Ujerumani imepata zaidi ya euro bilioni 1.15 kutokana na mauzo ya wachezaji.

Klabu hiyo imedumisha sifa yake kama klabu inayouza msimu huu wa majira ya joto kwa kumuuza mmoja wa wachezaji bora wa klabu hiyo, Jude Bellingham kwenda Real Madrid kwa kitita cha euro milioni 103 pamoja na nyongeza.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England kuhamia Klabu ya Madrid kumemfanya kuwa mchezaji wa pili ghali zaidi aliyesajiliwa katika dirisha la usajili la majira ya joto 2023 hadi sasa baada ya Declan Rice aliyejiunga na Arsenal kwa kitita cha euro milioni 105 akitokea West Ham United. Bellingham pia anakuwa mchezaji wa pili kuondoka Dortmund kwa gharama ya juu zaidi nyuma ya Ousmane Dembele ambaye aliuzwa kwenda Barcelona kwa euro milioni 140.

Timu hiyo inayotumia jezi nyeusi na njano pia imetengeneza euro milioni tano kutokana na mauzo ya Ansgar Knauff kwenda Eintracht Frankfurt.

**#2. RB Leipzig - Euro Milioni 133.50**

Klabu nyingine yenye mapato mengi zaidi kufikia sasa ni RB Leipzig. Washindi hao wa Kombe la DFB-Pokal wa mwaka 2023, wamewauza nyota wao wawili muhimu ambao ni Christopher Nkunku na Dominik Szoboszlai.

Nkunku aliuzwa kwa Chelsea kwa euro milioni 60 huku Szoboszlai raia wa Hungary akisajiliwa na Liverpool kwa ada ambayo ni rekodi ya klabu ya euro milioni 70. Golikipa, Fringe Josep Martinez pia alikamilisha uhamisho wa euro milioni 3.50 kwenda Klabu ya Genoa ya Ligi Kuu Italia, Serie A.

**#1. Chelsea - Euro Milioni 220.80**

Si jambo la kushangaza kwa 'Blues' kuongoza kwenye orodha hii baada ya wachezaji wanane wa kikosi cha kwanza kuondoka hadi sasa msimu huu wa majira ya joto. Baada ya kutumia zaidi ya euro milioni 600 kwenye dirisha lililopita la majira ya joto, klabu hiyo ya London ilihitaji kupunguza kikosi chao kilichokuwa kimejaa wachezaji.

Haja ya kuijenga upya timu pia ikawa muhimu kufuatia msimu wa kukatisha tamaa wa 2022-23. Zaidi ya hayo, ili kuepuka kukiuka sheria za FFP, Chelsea ililazimika kuwauza baadhi ya wachezaji wao bora ili kuweza kufanya usajili mpya.

'The Blues' hao wametengeneza jumla ya euro milioni 220.80 kufikia sasa kutokana na mauzo ya wachezaji msimu huu wa majira ya joto. Kai Havertz, Mason Mount, na Mateo Kovacic waliuzwa kwa wapinzani wao wa Ligi Kuu England, Arsenal, Manchester United, na Manchester City kwa ada ya jumla ya euro milioni 163.3.

Ziada ya euro milioni 57.5 pia imepatikana kutokana na mauzo ya Kalidou Koulibaly, Edouard Mendy, na Ruben Loftus-Cheek. Chelsea bado wanaweza kupata mapato zaidi kutokana na uwezekano wa kuondoka kwa Christian Pulisic na Hakim Ziyech. Mawinga wote wawili wamehusishwa na uhamisho wa kwenda klabu nyingine msimu huu wa majira ya joto.

## Nukuu

"Hatimaye nina furaha sana kuwa Barcelona na kujiunga nanyi. Natarajia sana msimu mzuri na mchezo wa kwanza. Ni ndoto kuwa Barca. Nakumbuka nikiwa mtoto nilimuona Rijkaard [Frank] na Pep [Guardiola] Barca. Mimi ni shabiki wa Barca, mara zote niliwafuatilia kwa karibu kila msimu na nina furaha sana na kujivunia kuwa sehemu ya timu hii," **kiungo mpya wa Barca, Ilkay Gundogan, akielezea furaha yake baada ya kujiunga na klabu hiyo akitokea Manchester City.**



"Nimekuwa nikiiangalia Arsenal kwa misimu michache iliyopita na mwenendo ambao wamekuwa wakiendelea. Si msimu uliopita, lakini msimu uliopita kabla, walimaliza nafasi ya tano, lakini unaweza kuona mtindo wa uchezaji wa Mikel [Arteta] alikuwa akiutekeleza. Msimu uliopita ulikuwa msimu bora, na kupeperusha kila timu nje ya maji isipokuwa Man City. Pamoja na Mikel na jinsi anavyofanya kazi, kikosi, jinsi kila mtu ni mchanga, nguvu karibu na klabu na pia changamoto ya kurudisha Arsenal mahali inapostahili, hiyo ina maana kubwa kwangu..." **Kiungo mpya wa Arsenal, Declan Rice, akielezea kwa nini amechagua kujiunga na timu hiyo akitokea West Ham United.**




"Miaka 10 iliyopita, nilipoanza safari yangu ya kujenga timu mpya huko Miami, nilisema kwamba nina ndoto ya kuleta wachezaji wakubwa zaidi ulimwenguni kwenye jiji hili la kushangaza. Wachezaji walioshiriki matarajio niliyokuwa nayo nilipojiunga na LA Galaxy kusaidia kukuza soka nchini Marekani na kujenga historia kwa kizazi kijacho katika mchezo huu tunaoupenda sana. Leo ndoto hiyo imetimia. Sikuweza kujivunia kwamba mchezaji wa kiwango cha Leo [Messi] atajiunga na klabu yetu, lakini pia nina furaha kumkaribisha rafiki mzuri, mtu wa ajabu na familia yake nzuri kujiunga na jumuiya yetu ya Inter Miami," **David Beckham akimkaribisha Lionel Messi, baada ya kujiunga na Inter Miami.**



“Miaka 10 iliyopita, nilipoanza safari yangu ya kujenga timu mpya huko Miami, nilisema kwamba nina ndoto ya kuleta wachezaji wakubwa zaidi ulimwenguni kwenye jiji hili la kushangaza. Wachezaji walioshiriki matarajio niliyokuwa nayo nilipojiunga na LA Galaxy kusaidia kukuza soka nchini Marekani na kujenga historia kwa kizazi kijacho katika mchezo huu tunaoupenda sana. Leo ndoto hiyo imetimia...

Ukurasa 13



DABO

# KLABU 5 LIGI KUU BARA ZITAKAZOANZA MSIMU NA MAKOCHA WAPYA

**Na Adam Fungamwangoo**

MAANDALIZI ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/24, yameanza kwa kila timu, zingine zikiamua kuondoka nchini kwenda kufanya ‘pre season’ maeneo ya mbali na walipozoea.

**Prisons huenda ika piga kambi, Dar es Sa laam, Zanzibar, au Arusha, Azam ikienda nchini Tunisia na Sim ba ikitoka nje ya bara la Afrika kwenda Ulaya, nchini Uturuki.**

Mabingwa wa Tanzania Bara Yanga wameamua kubaki nchini, Jiji la Dar es Salaam na bado baadhi ya klabu hazijaweka vizuri mipango yao kama zitakuwa wapi kujiandaa na msimu mpya.

Wakati baadhi ya timu zikiongozwa na Simba zitakuwa na makocha wale wale zilizokuwa nao msimu uliopita, kuna zingine zitakuwa na makocha wapya baada ya kuachana na makocha wao wa msimu uliopita kwa sababu mbalimbali.

Baadhi wamemaliza mikataba yao na kuamua kuondoka, wengine walitimuliwa na baadhi pamoja na kumaliza na timu hizo, lakini wameonekana hawatoshi kuelekea msimu ujao wa ligi.

Zifuatazo ni baadhi ya timu zitazoanza Ligi Kuu Tanzania Bara zikiwa na makocha wapya kabisa, pamoja na majina ya makocha hao...

**Azam FC - Youssouph Dabo**

Raia huyu wa Senegal ndiye kocha wa kwanza mpya kutangazwa na klabu nchini kwa ajili ya msimu ujao wa ligi.

Azam FC ilimtangaza Mei Mosi mwaka jana kabla hata ya kumalizika kwa msimu uliomalizika kuwa atakinoa kikosi hicho kwa msimu ujao.

Dabo akapata nafasi ya kukiangalia kwenye mechi kadhaa zilizobaki na kuwafahamu wachezaji ambao atakwenda kuwanoa.

Akaomba uongozi usifanye usajili mkubwa sana usiozidi wachezaji wanne kwani alichogundua ni kwamba timu ina wachezaji wazuri waliokosa mafunzo bora.

Kwa sasa yupo nchini Tunisia na kikosi chake kukitengeneza kwa ajili ya mikikimikiki ya mashindano yote atakayokabiliana nayo msimu ujao.

**Yanga - Miguel Gamondi**

Mwishoni mwa mwezi Juni Yanga ilimtangaza kocha wake mpya, Miguel Angel Gamondi kuchukua nafasi ya Nasreddine Nabi ambaye mkataba wake ulifikia tamati na hakutaka tena kuongeza kwa madai ya kwenda sehemu nyingine kutafuta changamoto.

Yanga inaweza kupata faida kubwa kwa kocha huyo raia wa Argentina kutokana na kulijua vilivyo soka la Kiafrika akifundisha kwa zaidi ya miaka 20 na kikubwa zaidi amezifundisha klabu kubwa ambazo kazi yao kubwa ni kusaka mataji na siku zote zinaishi kwenye hatua za makundi ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.

Timu hizo ni Wydad Casablanca ya Morocco, Esperance ya Tunisia, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, CR Belouizdad na USM Alger za Algeria ambayo kwa sasa ndiyo Mabingwa wa Kombe la Shirikisho Afrika.

“Nimepata mafanikio mazuri nikiwa na timu hizo, nimefurahi sana kujiunga na klabu kubwa kama Yanga na yenye historia nzuri kwenye soka la Tanzania na Afrika, kwangu ni klabu kubwa yenye mashabiki wengi wenye upendo, ninaamini kama tutaunganisha nguvu zetu pamoja na wanachama, mashabiki, viongozi na benchi la ufundi, wachezaji na wafanyakazi wengine, tutaendelea kupata mafanikio makubwa kuanzia pale tulipoishia,” akasema kocha huyo.

**KMC - Abdulhamid Moalin**

Katika kile kinachoonesha kuwa hataki masihara msimu ujao, viongozi wa KMC wamemchukua aliyekuwa Kocha wa Azam, Abdulhamid Moalin, kufundishia kikosi chao.

KMC ilikuwa moja ya timu zilizolazimika kushinda kwa lazima mechi chache zilizobaki za Ligi Kuu ili kuwa salama kushuka au kucheza ‘play off’ na kufanikiwa inaonekana haitaki tena kuishi kwenye hali hiyo msimu ujao.

“Nashukuru Mungu kwa kupata nafasi nyingine tena ya kuifundisha timu ya Tanzania, pia nashukuru uongozi wa KMC kwa kuniamini kuiongoza klabu yao, huu ni mtihani mkubwa kwangu kwenda kuifanya kuwa timu yenye kikosi imara, najua ligi kwa sasa nchini ni ngumu na hata msimu ujao haitokuwa rahisi, lakini nimekuja hapa na nimekubali nikijua haya yote,” anasema Moalin.

Anachukua nafasi ya Jamhuri Kihwelo ambaye aliichukua timu hiyo ikiwa kwenye hali mbaya katika Ligi Kuu, na kufanikiwa kuibakisha akicheza mechi nne za ligi pamoja ya ‘play off’ dhidi ya Mbeya City,

Moalin alikuwa Kocha Mkuu tangu Azam kuanzia Januari mwaka jana aliporithi mikoba ya George Lwandamina, lakini mwisho wake naye ulikuwa Agosti mwaka jana.

**Mwinyi Zahera - Coastal Union**

Klabu ya Coastal Union nayo haijapoa, imemtangaza Mwinyi Zahera, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kuwa Kocha Mkuu, akichukua nafasi ya Elius Fikiri ambaye benchi lake la ufundi na yeye akiwa ndani lilivunjwa na Kamati ya Utendaji ya klabu hiyo kwenye Mkutano Mkuu uliofanyika hivi karibuni jijini Tanga.

Zahera ambaye atachukua jukumu la kukinoa kikosi hicho, ametokea Klabu ya Polisi Tanzania ambayo imeshuka daraja msimu uliomalizika.

Kocha huyo aliingia nchini mwaka Aprili 2017 na kuwa Kocha Mkuu wa Yanga, akiifundisha kwa kipindi cha miezi isiyopungua 15 akaonyeshwa mlango wa kutokea, Oktoba 1918 na nafasi yake ikachukuliwa na Charles Boniface Mkwasa.

**Fred Felix Minziro - Prisons**

Kocha aliyeifundisha Geita Gold msimu uliopita, Fred Felix Minziro anakwenda kuwa Kocha Mkuu wa Prisons kwa msimu ujao baada ya kutambulishwa rasmi.

Minziro anakwenda kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Mohamed Abdallah ‘Bares’ aliyetimkia Mashujaa FC.

Kihistoria hii si mara ya kwanza kwa kocha huyo kuwafundisha Maafande hao kwani ameshawahi kuwa kocha mkuu mara kadhaa katikati ya miaka ya 1990 na hata mwanzoni mwa miaka ya 2000, hivyo ni kama anarejea nyumbani.

**JE, WAJUA?**



KWA mujibu wa mtandao wa ESPN, hawa ndio viungo washambuliaji 10 bora kwa sasa; Kevin De Bruyne (Man City), Martin Ødegaard (Arsenal), Bernardo Silva (Man City), Jamal Musiala (Bayern,) Bruno Fernandes (Man United), Julian Brandt (Dortmund), Gavi (Barca), Brahim Díaz (Madrid), Lucas Paqueta (West Ham) na Nicolo Barella (Inter).



# Hati za kimila 500,000 kusajiliwa katika h/shauri sita

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia mradi wa Uboreshaji Usalama wa Miliki za Ardhi (LTIP) inakusudia kupanga, kupima na kusajili hati za hakimiliki za kimila 500,000 kwa halmashauri sita nchini.

Katika mradi huo Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma inatarajia kunufaika kwa kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi katika vijiji 60.

Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya, alibainisha hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa wadau kujadili mpango wa matumizi ya ardhi wilayani hapa.

Msuya alisema Wizara ya Ardhi iliichagua Chamwino kuwa miongoni mwa wilaya sita ambazo ni Mufindi, Songwe, Mbinga, Maswa na Longido.

"Mradi huu kwa wilaya hizi sita umelenga kuboresha usalama wa miliki za ardhi kwa kupanga, kupima na kusajili hati za hakimiliki za kimila 500,000 ambapo Wilaya ya Chamwino inakusudiwa kunufaika na mradi huu kwa kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ya wilaya kwa vijiji 60."

"Mradi huu umeanza kutekelezwa na halmashauri yetu na ndiyo maana leo tumekutana hapa ili kujadili rasimu na hatimaye tuweze kupitisha rasimu hii na kuwa mpango wa matumizi ya ardhi ya Wilaya ya Chamwino," alisema.

Aidha, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino inakabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo yameibuliwa katika rasimu ya mpango huo ikiwamo ukosefu wa usalama wa miliki za ardhi, ukuaji wa kasi wa miji vijiji usiodhibitiwa,

Alisema matatizo mengine ni ukuaji wa mji wa Chamwino kuelekea katika ardhi za vijiji, upotevu wa bionuai na uharibifu wa mazingira, uzalishaji mdogo wa mazao ya kilimo na ufugaji na uhaba wa malisho ya mifugo.

Alieleza tatizo lingine ni mfumo dhaifu wa ukusanyaji na utupaji taka ngumu na taka, ubovu wa bararaba katika baadhi ya maeneo, uhaba wa maji kwa baadhi maeneo, upungufu wa baadhi ya huduma za jamii kama vile shule za msingi, sekondari, zahanati na vituo vya afya kwa baadhi ya maeneo.

Meneja Urasimishaji Ardhi ya Vijiji kupitia mradi huo, Joseph Osana, alisema mradi umelenga kuboresha usalama wa miliki za ardhi kwa kupanga, kupima na kusajili miilki za ardhi zipatazo milioni 2.5 ambazo zinazojumuisha hati miliki 1,000,000 na leseni za makazi 1,000,000 katika maeneo ya mijini na hati za hakimiliki za kimila 500,000 vijijini.




Mfanyabiashara kutoka Kurasini, Peter Okoka Mwasandube (kushoto), akipokea mfano wa hundi wa 1,000,000/- kutoka kwa Balozi wa Kampeni ya Cha Wote, Millard Ayo (kulia), baada ya kuibuka mshindi wa kampeni hiyo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yapiga 'stop' w'biashara kuuza mazao bila kusajiliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetahadharisha kumeibuka kwa wimbi la matapeli wa mitandaoni kwenye sekta ya kilimo, ikisema kuna baadhi ya wafanyabiashara wameshatapeliwa mazao ya Sh. bilioni mbili.

Hivyo, imesema kutokana na hali hiyo kuanzia sasa hakuna mfanyabiashara yoyote atakayeruhusiwa kuuza mazao bila kuwa na kampuni iliyosajiliwa na kutambuliwa na Wizara ya Kilimo.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye mkutano wa wafanyabiashara na wadau wanaouza mazao ndani na nje ya nchi, uliofanyika jijini hapa.

Alisema matapeli hao wamekuwa wakitangaza biashara hiyo kwenye mitandao ya kijamii kama instagram na facebook kuwa wanachukua zabuni za ununuzi wa mazao na kuwaomba fedha ya awali kwa wafanyabiashara wanunuzi wa mazao na kutokomea nazo bila kurudisha mrejesho wowote kwa wafanyabiashara.

Bashe alisema serikali imechukua hatua kuhakikisha mfanyabiashara lazima awe na kampuni inayotambulika na kwa upande wa wafanyabiashara wageni nao wanapaswa kusajili kampuni na kama itashindikana basi washirikiane na wafanyabiashara wa ndani ambao wana kampuni ili kuendesha biashara hiyo.

Alisema: "Tumeamua kufanya hivyo ili kuondoa utapeli unaoendelea katika mitandao kupitia baadhi ya kampuni nawaonya wafanyabiashara kuwa makini na suala hili kuna wafanyabiashara wameshatapeliwa mazao ya Sh. bilioni mbili," alisema Bashe.

Waziri Bashe alisema biashara ya mazao ya kilimo haiko rasmi jambo ambalo linachangia kuikosesha taifa kodi na fedha za kigeni, ndiyo maana wameanza kuisuka ili iwe rasmi.

Kadhalika, alisema serikali inatarajia kuhifadhi tani milion tatu za mazao ya chakula, huku akisisitiza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) inatakiwa kutafuta masoko.

Alisisitiza kuwa serikali haijazuia kuuza mazao nje isipokuwa watu wanatakiwa kufuata utaratibu ili kuhakikisha wanafanya biashara hiyo ipasavyo kama zilivyo biashara nyingine.

Katika hatua nyingine, Waziri Bashe alisema serikali inatarajia kuanza kusajili maghala yote ya sekta binafsi ili kusaidia kujua taifa lina chakula kiasi gani.

Alisema wanatarajia kutangaza zabuni ya uzalishaji mbegu, huku akisisitiza sekta binafsi ijitokeze, kuongeza kuwa ifikapo mwaka 2025 mashamba 17 ya serikali yatakuwa ya kilimo cha umwagiliaji.

# 'Wazazi hamasisheni watoto kushiriki mashindano ya insha'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa rai kwa wazazi kuwahamasisha wanafunzi kushiriki mashindano ya uandishi wa insha kwa nchi za Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa kuwa yanawaandaa vyema kwenye mitihani yao ya mwisho.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, alitoa rai hiyo juzi kwenye hafla ya utoaji tuzo kwa wanafunzi walioshinda mashindano hayo kwa mwaka 2021 jijini hapa.

"Mashindano haya yanasaidia wafanye vizuri kwenye mitihani yao ya kitaifa uzoefu umeonesha hivyo, sasa tuwahamasishe washiriki tuna wanafunzi wengi sana wenye uwezo wa kushiriki mashindano haya," alisema.

Alisema uandishi wa insha ni sehemu ya mafunzo na inawajengea wigo mpana wa kujifunza masuala muhimu yanayohusu jumuiya hizo.

"Ili kuandika insha iliyobora kitu cha kwanza ni kufanya utafiti ukusanye taarifa mbalimbali za kile unachoandika na hawa wanafunzi wamefanya hivyo, hawa vijana wetu wamejidhihirisha pamoja na changamoto ya elimu yetu lakini haipo mbaya kama watu wanavyosema, elimu yetu bado ni nzuri na ina uwezo wa kuhimili kitaifa na kimataifa," alisema.

Prof.Mdoe alisema mashindano hayo ni sehemu ya mkakati mkubwa wa EAC na SADC katika kujenga uelewa wa wanafunzi kuhusu kazi na mipango ya jumuiya, hivyo ni vyema kuwahamasisha wakashiriki kwa wingi na kuwaunga mkono.

Alisema kwenye mashindano ya SADC walijitokeza wanafunzi 130 na wamepatikana washindi 10 na kwa EAC walishiriki 315 wamepatikana washindi 10.

Awali, akisoma risala ya mashindano hayo, Mratibu wa Insha wa Wizara hiyo, Matuha Massati, alitoa wito kwa walimu na wazazi kuwahimiza wanafunzi kushiriki katika mashindano hayo na mengine kutokana na uzoefu kuonesha washiriki hufanya vizuri kwenye mitihani yao ya mwisho ya kuhitimu kidato cha nne na sita.

Alisema: "Wanafunzi 130 walishiriki kwenye shindano la uandishi wa insha za SADC kwa mwaka 2021 na baada ya kusahihishwa walipatikana washindi 10 ngazi ya taifa ambao wote watapewa zawadi na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, hatua hii italeta hamasa ya uandishi wa insha".

Aliongeza: "Kwa EAC insha bora hupelekwa makao makuu ya jumuiya na kushindanishwa na nchi wanachama wa jumuiya hiyo ambapo wanafunzi 315 kwa mwaka 2021 walishiriki shindano".



# Madereva saba wafungiwa leseni kisa uzembe barabarani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limewafungia leseni za udereva madereva saba wa mabasi ya abiria kutokana na makosa mbalimbali ya ukiukaji wa sheria za usalama barabarani katika kipindi cha nusu mwaka.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni mbalimbali zilizofanywa na jeshi hilo kuanzia mwezi Januari mpaka Julai.

Kamanda kuzaga aliyataja mabasi ambayo madereva wake walifungiwa leseni katika kipindi hicho kuwa ni pamoja na New Force, Zanuni, Rungwe Express, Super Rojas, Abood Bus Service na Kyela Express.

Alisema madereva wa mabasi hayo walikamatwa kwa nyakati tofauti na kuchukulia hatua za kufungiwa leseni zao za udereva kwa kipindi cha kati ya miezi miwili na mitatu na wengine kufikishwa mahakamani.

"Miongoni mwa makosa ya usalama barabarani yaliyoripotiwa kufanywa na madereva hao ni pamoja na kuendesha magari kwa mwendo kasi, kusababisha ajali za vifo, kujeruhi na kuharibu magari na miundombinu ya barabara," alisema Kamanda Kuzaga.

Aidha, Kamanda Kuzaga aliwataka madereva kufuata sheria na kanuni za usalama barabarani ili kuepuka ajali zinazoweza kuepukika.

Alisema jeshi hilo litaendelea kuta elimu na mafunzo ya kuwajengea uwezo madereva kwa kushirikiana na vyuo mbalimbali vya udereva vilivyoko mkoani humo.

Aliwataka abiria wa mabasi kutoa taarifa haraka kwa Jeshi la Polisi wanapoona madereva wanakiuka sheria za usalama barabarani hasa kuendesha magari kwa mwendokasi ili hatua zichukuliwe mapema.

Alisema ajali zinapotokea zinasababisha madhara mbalimbali kwa abiria na mali zao ikiwa ni pamoja na vifo, majeraha na ulemavu wa kudumu.

Miaka ya karibuni Mkoa wa Mbeya uligubikwa na wimbi la ajali za mara kwa mara hasa kwenye maeneo yenye milima na miteremko mikali hali iliyolilazimu Jeshi la Polisi kuanzisha utaratibu wa magari makubwa na madogo kupita kwa awamu.

Maeneo ambayo utaratibu huo unatumika ni pamoja na kwenye mteremko wa Mlima Iwambi, eneo la Mlima Inyala na kwenye mteremko wa Senjele mkoani Songwe.

# Uboreshaji miundombinu waanza kuvutia wawekezaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UBORESHAJI wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji unaotekelezwa na serikali mkoani Mbeya, umeanza kuvutia wawekezaji wa nje kwenye sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya viwanda.

Mwishoni mwa wiki mwekezaji mmoja mwenye asili ya India alikabidhiwa eneo lenye ukubwa wa ekari 100 na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha nondo na bidhaa mbalimbali za chuma.

Mwekezaji huyo alikabidhiwa eneo hilo lililopo kwenye mashamba ya kilichokuwa kiwanda cha kuzalisha nyama cha Tanganyika Pakers katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Akizungumza baada ya kuonyeshwa eneo hilo, mwekezaji huyo mbaye anaitwa, Rajendra Postimset alisema alivutiwa kuwekeza kiwanda hicho baada ya kubaini kuwa eneo lipo jirani na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA).

Alisema mbali na kuwa jirani na uwanja huo, pia kuna miundombinu ya barabara inayounganisha eneo hilo na uwanja huo ambayo itamrahisishia kusafirisha vitu mbalimbali kutoka na kuingia kwenye kiwanda hicho.

Alisema kwa muda mrefu alikuwa anatafuta eneo ndani ya Tanzania ambapo TIC walimpeleka katika mikoa mbalimbali ikiwamo Mtwara, Ruvuma na Songwe lakini hakuridhika na maeneo hayo kutokana na miundombinu kutokuwa imara.

"Hiki kiwanda nakusudia kuwekeza Dola za kimarekani milioni 50 (zaidi ya Sh. bilioni 115 za kitanzania) kwa hiyo naishukuru Serikali ya Tanzania kwa kunipatia eneo hili na nategemea tutaendelea kushirikiana vizuri," alisema Rajendra.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri alisema mwekezaji huyo alikuwa anahitaji ekari 200 kwa ajili ya uwekezaji huo lakini wakaamua kumpatia ardhi hiyo kwa awamu kulingana na mahitaji. Alisema walikubaliana kuanza na ekari hizo 100 lakini baada ya kuanza uwekezaji watamtafutia ekari zingine 100 ili kufikia lengo lake hilo la kupata ekari 200.

Teri alisema kiwanda hicho kitakuwa kikubwa na hivyo kuongeza ajira kwa Watanzania, kukuza mapato ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya na taifa kwa ujumla.

"Kwa sasa tupo kwenye utaratibu wa kumsajili kwenye kituo chetu ili awe miongoni mwa wawekezaji kwenye mkoa huu, lakini kiwanda hiki kitawasaidia wananchi wa Mbeya na mikoa jirani kupata vifaa vya ujenzi hapahapa badala ya kufuata Dar es Salaam," alisema Teri.

Kaimu Meneja wa TIC Mkoa wa Mbeya, Deusdedit Hokororo, alisema watahakikisha wanamlinda mwekezaji huyo kwa kuhakikisha anapata mahitaji yote muhimu ili uwekezaji huo uwe endelevu.

Alisema kwa mujibu wa maelezo ya mwekezaji huyo ni kwamba uwekezaji huo ni wa mwaka mmoja na hivyo kuna uwezekano fedha zikaongezeka mwaka hadi mwaka.

Kiwanda hicho cha nondo kitakuwa ndicho kiwanda cha kwanza cha chuma kujengwa mkoani Mbeya na kinatarajiwa kuwa miongoni mwa viwanda vikubwa mkoani humo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Uturo, Kata ya Mapogoro wilayani Mbarali mwishoni mwa wiki alipokwenda kuzindua ununuzi wa mpinga unaonunuliwa na serikali kupitia Wakala wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). **PICHA: NERBAT MSOKWA**

# Hospitali za rufani zatakiwa kuwajengea uwezo watumishi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI za rufani za mikoa na za kanda zimetakiwa kuweka utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi wa afya wanaofanya kazi kwenye zahanati na vituo vya afya kwa lengo la kuboresha huduma za afya.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kukagua uboreshaji wa miundombinu ya afya katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Alisema serikali imewekeza fedha nyingi kwenye ujenzi wa zahanati katika kila kijiji na vituo vya afya kwenye kila kata, ununuzi wa vifaa tiba lakini katika baadhi ya maeneo bado huduma hazijaimarika.

Alisema ili kuimarisha huduma hizo, wataalamu wa hospitali za rufani za mikoa na za kanda wanatakiwa kwenda kuwapatia mafunzo watumishi wa maeneo hayo ili huduma ziwe bora zaidi.

"Hili linatakiwa kuratibiwa na Mganga Mkuu wa Mkoa, kuna baadhi ya vifaa tumenunua na kuviweka kwenye hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati lakini watumishi wa maeneo hayo hawana uzoefu navyo, ni wajibu wenu kwenda kuwajengea uwezo," alisema Dk. Grace.

Alisema kwa sasa Tanzania imepiga hatua kubwa kwenye matibabu ya kibingwa na kwamba imeyaacha mbali baadhi ya mataifa jirani ambayo wananchi wake wanalazimika kuvuka mipaka kufuata huduma.

Alisema katika Hospitali ya Kanda Mbeya kuna maboresho mbalimbali ambayo yamefanywa ili kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi mahitaji. Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji aliishukuru serikali kwa uwekezaji ambao inaendelea kuufanya kwenye hospitali hiyo akieleza kuwa unasaidia kuboresha huduma.

Alisema kwa sasa serikali imenunua mashine ya MRI kwa ajili ya kuwasogezea huduma wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na wa nchi jirani ambao walikuwa wanalazimika kwenda katika Hospitali ya Taifa Mhimbili (MNH).

"Sisi hapa tunafanya kazi kwa ushirikiano na tunahakikisha tunaboresha huduma zetu kila siku, lakini tunao wajibu wa kuzisaidia hospitali za mikoa na za wilaya ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma zilizo bora," alisema Dk. Mbwanji.

Alisema watahakikisha wanaendelea kutekeleza maagizo mbalimbali waliyopewa na Naibu Katibu Mkuu huyo hasa la kuzijengea uwezo hospitali za ngazi za chini.

Wiki iliyopita Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alizindua mashine ya MRI ambayo ni mara ya kwanza kuwapo katika hospitali hiyo ya kanda na kuagiza itumike vizuri ili idumu kwa muda mrefu.

Katika miaka ya karibuni serikali imekuwa ikiboresha huduma za afya katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya ambapo baada ya kusimika mashine za CT-Scan na MRI huduma zote za kibingwa zinapatikana.





# SMZ yaingia makubaliano mkopo Bil. 470/- NBC

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imekamilisha makubaliano ya kupata mkopo wa ushirikiano wenye thamani ya takribani Sh. bilioni 470 (dola za Marekani milioni 200) kutoka Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) na washirika.

Mkopo huo wa miaka minane utaisaidia SMZ kutekeleza miradi mbalimbali ya kuboresha huduma za jamii na miundombinu.

Akizungumza baada ya utiaji saini mkataba wa mkopo huo jana, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliipongeza Benki ya NBC kwa kufanikisha ukamilishaji wa mkataba wa utoaji wa mkopo huo.

"Ninaipongeza Benki ya NBC kwa jitihada zake za kukamilisha taratibu za mkopo huu kwani utasaidia kuboresha uchumi wa Zanzibar," alisema.

Dk. Mwinyi alisema mkopo huo utaleta mageuzi makubwa katika kuboresha utoaji wa huduma za kijamii pamoja kuboresha miundombinu, kuongeza ajira na kuchochea maendeleo endelevu kwa kuwa unakwenda sambamba na mikakati ya serikali yake katika kutekeleza dira ya maendeleo.

Dk. Mwinyi alisema fedha za mkopo huo zitaelekezwa katika miradi ya huduma za jamii na miundombinu ikiwamo sekta ya afya, taasisi za elimu, kujenga mitandao ya miundombinu na miradi mbalimbali ya maendeleo ya jamii.

"Kwa kuwekeza katika sekta hizi muhimu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusudia kuboresha maisha, kukuza utoaji wa huduma muhimu za jamii na kuchochea ukuaji wa uchumi," Rais Dk. Mwinyi alisema.

Benki ya NBC ni mwandaaji, mtoaji na wakala mkuu wa dhamana wa mkopo huo kwa kushirikiana na benki zingine za ndani.

"Mkopo huu ni muhimu katika kugharamia uboreshaji wa huduma za jamii na miundombinu ambao utaboresha maisha ya wazanzibari na kuchochea ukuaji wa uchumi," NBC ilibainisha katika taarifa yake ya jana.

"Tukiwa kama wataalamu wa mikopo ya ushirikiano, Benki ya NBC itashirikiana na Serikali ya Zanzibar kuleta mageuzi chanya, kuchochea maendeleo endelevu na kuboresha maisha ya wananchi," uongozi wa benki hiyo ulieleza kupitia taarifa hiyo.

Akizungumza wakati wa utiaji wa saini wa mkataba wa mkopo huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema amefarijika na jitihada za benki yake katika kusaidia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya ukuaji jumuishi wa maendeleo ya kiuchumi.

Mkurugenzi huyo alisema uandaaji wa mkopo huo unathibitisha ushiriki wa benki yake katika kuwa na malengo jumuishi ya uchumi endelevu na uboreshaji wa maisha ya watu.

"Benki ya NBC imejizatiti katika kuchochea gurudumu la maendeleo na uboreshaji wa utoaji wa huduma za jamii kupitia uwajibikaji wa utoaji wa huduma za fedha na uchocheaji wa ukuaji uchumi," alisema.

Aliongeza kuwa Benki ya NBC ni kongwe, inatoa huduma bunifu za kifedha katika sekta mbalimbali za uchumi ikiwamo kusaidia serikali katika uboreshaji wa huduma za kijamii.

Kwa mujibu wa ripoti za Benki Kuu ya Tanzania (BoT), uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 6.8 mwaka 2022, zaidi ya matarajio ya ukuaji wa asilimia 5.4, kutokana na ukuaji wa sekta ya utalii na uwekezaji wa umma na watu binafsi.

## Serikali kushawishi vijana, wanawake kupenda kilimo

**Na Rahma Suleimman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Misitu, imesema itaendelea kutumia mbinu mbalimbali kushawishi vijana na wanawake kushiriki kwenye kilimo, ili kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira nchini.

Waziri wa wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maonyesho ya Sikukuu ya Wakulima (nane nane) itakayoadhimishwa katika viwanja vya Dole Kizimbani mwezi ujao.

Shamata alisema kuwa maonyesho hayo ni jukwaa muhimu kwa wakulima na wadau wa sekta ya kilimo kupata taarifa, maarifa na ujuzi unaochochea ushiriki wao kwenye kilimo, lakini pia kuongeza uzalishaji wa mazao.

"Kupitia maonyesho hayo wadau watajifunza mbinu na teknolojia mpya za kuongeza uzalishaji lakini pia kujiunga na shughuli za kilimo na kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao yanayozalishwa, hivyo kukifanya kilimo kuendelea kuwa na tija kwa maisha ya watu na uchumi wa nchi," alisema Shamata.

Aidha, alisema kaulimbiu ya maonyesho ya mwaka huu ni 'Vijana na wanawake ni msingi imara wa mifumo endelevu ya chakula' ambayo inalenga kutambua mchango wa vijana na wanawake katika kilimo.

Waziri huyo alisema kuwa ujumbe huo unalenga kutoa fursa zaidi kwa vijana na wanawake kujiekeza katika sekta ya kilimo kwa manufaa yao wenyewe, familia zao na kwa taifa kwa jumla kwa kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza utegemezi.

Akizungumzia mikakati ya wizara hiyo katika kuinua kilimo nchini, Shamata alisema serikali imeongeza bajeti ya kilimo ambayo kwa mwaka 2023/2024 imeongezeka hadi kufikia Sh. bilioni 98.7 kutoka Sh. bilioni 53.5 mwaka 2022/2023.

Alieleza mkakati mwingine ni kuongeza upatikanaji wa vifaa na nyenzo za kilimo zitakazowavutia vijana na wanawake kushiriki kwenye shughuli za kilimo, kuongeza idadi ya watalii katika hifadhi hadi kufikia watalii 100,000 kutoka 64,000 kwa mwaka 2022/2023.




Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Hussein Gulam (kushoto), akizindua mwongozo wa utoaji mikopo ya elimu ya juu jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo Zanzibar, Idd Haji na (wa pili kulia) ni Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Khalis Masoud. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZHELB kuwashtaki wanafunzi waliokacha kufanya marejesho

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB) inatarajia kuwafikisha katika Mamkala ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) wadaiwa sugu walioshindwa kufanya marejesho ya fedha walizokopeshwa.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa bodi hiyo, Iddi Khamis Haji, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika hafla ya uzinduzi wa mwongozo wa maombi ya upataji wa mikopo uliofanyika katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Mazizini.

Mkurugenzi huyo alisema kuna wanafunzi 12,000 ambao wamepata mikopo tangu mwaka 2011 hadi sasa na waliolipa wanakadiriwa kufikia 5,000, hivyo kuna pengo kubwa ya wale ambao hawajalipa.

"Dawa ya deni ni kulipa hivyo hatua ya kuwawajibisha kwa haraka ni kuwapeleka ZAECA na hatua zingine zitafuata ikiwamo kuwafikisha mahakamani," alisema.

Alisema wanachukua hatua za dharura kutoa taaluma kwa wale ambao hawajarejesha mkopo ili kurejesha mkopo huo na kuwapatia wengine wanaohitaji mkopo.

Aidha, alisema hali ya ukusanyaji madeni ni mzuri, kwamba kwa sasa wanakussanya mapato wastani wa Sh. milioni 460 kwa mwezi ambapo ni kiwango kizuri ikilinganishwa na nyuma walipokuwa wanakusanya wastani wa Sh. bilioni tano kwa mwaka mmoja.

Alisema mwaka jana kulikuwa na maombi 480 ya wanafunzi waliomba na waliokosa ni 100 lakini kwa mwaka huu bajeti iliyotengwa inatosha kuwapatia wanafunzi wote waliofaulu kidato cha sita kwa mwaka huu.

Alisema kwa mwaka huu wanatarajia kutoa mikopo kwa wanafunzi 2,400 na waliofaulu kidato cha sita mwaka huu ni 2,500, hivyo hawatarajii wale ambao wenye sifa kukosa mikopo.

Hivyo, aliwataka wanafunzi kuitumia fursa ya kuomba mkopo katika Bodi ya Mikopo ya Zanzibar na Serikali ya Muungano, kwamba mikopo hiyo haina riba.

Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Hussein Gulam, alisema kwa mujibu wa matokeo ya kidato cha sita yaliyotangwa hivi karibuni na Baraza la Mitihani Tanzania, wanafunzi wa Zanzibar waliofaulu mitihani hiyo ambao 2,570 wanasifa za kujiunga na elimu ya juu, kati ya wanafunzi 2,587 waliofanya mitihani hiyo.

Alisema wanafunzi hao waliofaulu kwa kiwango cha sita kwa daraja la kwanza hadi la tatu ni 2,570 na wote wana sifa ya kujiunga na masomo ya elimu ya juu.

Aliwapongeza walimu kwa kazi na juhudi kubwa waliyoifanya pamoja na wazee na walezi kwa ushirikiano wao na kufikia mafanikio hayo.

"Jambo hili sio la mtu mmoja serikali, walimu na wazee lazima kushikamana ili kupata mafanikio chanya, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wadau wa elimu maana ushirikiano wao umezaa matunda na kupata matokeo mazuri," alisema.

Gulamu alisema serikali imeongeza bajeti katika miundombinu ya elimu, bodi ya mikopo ya elimu ya juu na uendeshaji wa shughuli za elimu ili kuhakikisha sekta hiyo inafanya mageuzi makubwa.

Alisema ongezeko hilo la bajeti litasababisha maboresho ya maslahi mbalimbali, hivyo aliwataka wanafunzi wanaohitaji mikopo ya elimu ya juu kutumia fursa kwa bodi zote mbili ya Zanzibar na Serikali ya Muungano.

# Maelfu kunufaika na mradi wa maji uliofadhiliwa na SBL

**Na Mwandishi Wetu,** HANDENI

NAIBU Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, ameipongeza Kampuni ya Serengeti Breweries Limited (SBL) kwa mchango wake katika kufadhili miradi ya maji inayolenga kutoa majisafi na salama kwa Watanzania katika maeneo ya vijijini yenye upungufu wa maji.

Amesema ufadhili huo unaunga mkono mikakati ya serikali ya kuongeza upatikanaji wa majisafi na salama katika maeneo ya vijijini kufikia asilimia 85 ifikapo mwaka 2025.

Maryprisca alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki huko Kwamaizi wilayani Handeni, mkoani Tanga wakati wa hafla ya kukabidhi mradi wa bwawa la maji kwa Kata ya Kideleko baada ya kukamilika kwa mradi huo.

Utekelezaji wa mradi huo ulianza Februari mwaka huu kwa ushirikiano na WaterAid Tanzania na Wizara ya Maji kama watekelezaji wa kiufundi kwa msaada wa kifedha wa Sh. milioni 380 kutoka SBL.

Katika hafla hiyo, Maryprisca alisema serikali inafanya kazi kwa bidii kujenga, kukarabati na kupanua vyanzo vya maji ili kuboresha upatikanaji wa majisafi na salama katika maeneo ya vijijini, hivyo jambo ambalo SBL imefanya ni la kupongezwa kwa kuwa linakwenda sambamba na juhudi za serikali za kukabiliana na uhaba wa majisafi na salama katika maeneo ya vijijini.

"Nimefurahi kuona sekta binafsi ikiwa kinara katika kushughulikia masuala muhimu kama ukosefu wa majisafi na salama katika jamii zetu. Ni kutokana na azma ya SBL katika miradi ya maji kwamba wakazi wa Kijiji cha Kwamaizi sasa watakuwa na upatikanaji wa majisafi na salama bila malipo.

"Ninawapongeza sana SBL kwa kufadhili mradi huu kwa kiasi cha Sh. milioni 380, hivyo kuruhusu utekelezaji mafanikio wa miradi hii ndani ya miezi mitano tu," alipongeza Naibu Waziri Maryprisca na kuwashukuru Water Aid, Handeni Trunk Main na RUWASA kwa usimamizi wa utekelezaji wa mradi huo.

Naibu Waziri aliipongeza SBL na WaterAid kwa kwenda mbali zaidi kwa kutoa mafunzo kuhusu masuala yanayohusiana na huduma za usafi na maji (WASH) kwa wanawake wa Kwamaizi ili kuwapa ujuzi wa jinsi ya kusimamia bwawa la maji.

Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Dk. Obinna Anyalebechi alisema "ufadhili wa mradi wa Handeni na kampuni yetu ni sehemu ya nguzo moja ya msaada wa jamii ya SBL inayojikita katika kutoa huduma ya maji kwa jamii zilizopokonywa rasilimali hiyo. Inayojulikana kama 'Maji ya Uhai'.

"Programu hii inalenga kurejesha au kujaza upya jamii sawa na kila tone la maji linalotumiwa na kampuni yetu katika shughuli zake. Mwaka huu, kwa mfano, tuna jukumu la kurejesha mita za ujazo 87,000 za maji, sawa na jumla ya maji yanayotumiwa katika bia zetu tatu za bia huko Dar es Salaam, Moshi na Mwanza."

Aliongeza, "Tumeenda hatua ya ziada kwa kufadhili mafunzo ya maji na usafi (WASH) kwa wanawake walengwa katika eneo hili ambao sasa wana vifaa vya kutosha vya kushughulikia mradi huu na kuhakikisha kuwa unadumu kwa miaka mingi ijayo."

Mkurugenzi wa WaterAid nchini Tanzania, Anna Mzinga, alisema "SBL imekuwa mmoja wa washirika wetu muhimu katika utekelezaji wa miradi ya maji nchi nzima, utayari wao katika kusaidia kazi hii ni wa kuvutia. Kupitia ushirikiano wetu, zaidi ya Watanzania milioni mbili hasa katika maeneo ya vijijini kama Kwamaizi sasa wanapata majisafi na salama bila malipo."

Aliongeza: "Mradi wa usambazaji maji wa Bwawa la Kwamaizi ni mfano wa kile tulichokuwa tukifanya kwa miaka 40 iliyopita na kile tutakachokifanya kuendeleza malengo yetu.

"Lengo letu ni kusaidia kuleta maendeleo katika maisha ya watu, jamii na uchumi kwa kufanya maji, usafi na usafi wa mazingira kuwa jambo la kawaida kwa kila mtu, kila mahali."



Mdhibiti Ubora wa Shule wa Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam, Elikana Manyilizu, akimkabidhi cheti cha kuhitimu darasa la saba mwanafunzi wa Shule ya St Anne Marie Academy ya Mbezi kwa Msuguri kwenye mahafali ya 20 yaliyofanyika shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## DIT, TIKA zawanoa walimu kiteknolojia

**Na Maulid Mmbaga**

CHUO cha Teknolojia (DIT) kikishirikiana na Taasisi ya TIKA ya Uturuki, wameendesha programu ya mafunzo kwa walimu kutoka vyuo vinne nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo katika maeneo ya umahiri wa teknolojia.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam baada ya kuhitimisha mafunzo hayo ya siku tano, Mhadhiri na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni Tanzu DIT, Dk. John Msumba, alisema walimu hao ni kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Karume na DIT.

Msumba ambaye alikuwa mratibu wa programu hiyo, alisema mafunzo hayo yalilenga kuwaongeza uwezo walimu wa kutumia mashine za kisasa katika kuwafundisha wanafunzi, akieleza kuwa mapinduzi ya nne ya viwanda yanahitaji ujuzi wa kisasa katika kutatua matatizo mbalimbali.

"Ili wanafunzi waweze kuwa na huo ujuzi, lazima walimu wajengewe uwezo, kama mwalimu hana uelewa, mwanafunzi pia hataweza kufanya hivyo, ndiyo maana tumekuwa na mipango mingi kuhakikisha tunajengea walimu uwezo.

"Hii ni moja kati ya mafunzo muhimu sana ambayo yamefadhiliwa na wenzetu wa TIKA, kwa mafunzo haya walimu sasa wana uwezo wa kufundisha wanafunzi jinsi ya kutumia teknolojia za kisasa katika kutatua changamoto mbalimbali za jamii," alisema Msumba.

Alieleza kuwa wataendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa walimu na wanafunzi wakisimamiwa na TIKA. Serikali imewasaidia kuanzisha kituo mahiri kwa ajili ya TEHAMA, akieleza kuwa kinahitaji kikute wataalamu ambao tayari wanajua na wana utaalamu wa kutumia vifaa vya kisasa.

Balozi wa Uturuki nchini, Dk. Mehmet Güllüoğlu, alisema atahakikisha Tanzania na Uturuki zinaendeleza ushirikiano wa kimaendeleo hasa katika sekta za elimu, teknolojia, viwanda, kilimo, biashara na utamaduni.

"Tuna imani kwamba kupitia programu hii, wanafunzi wamenufaika kwa kusoma na kuongezwa uelewa juu ya vitu vingi, na tutaendelea kuendesha mafunzo mbalimbali kwa pamoja," alisema Güllüoğlu.

# Wasichana wanaoishi mazingira magumu wakabidhiwa bajaji 10

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amekabidhi bajaji 10 zenye thamani ya Sh. milioni 84 kwa wasichana na vijana wa kike wanaoishi katika mazingira magumu kupitia mradi wa Pink Ride uliobuniwa na kusimamiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Akizungumza mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam wakati wa kukabidhi bajaji hizo sambamba na uzinduzi wa mradi huo, aliipongeza TGNP kwa kuandaa na kuratibu mradi huo wa kuwainua wasichana kiuchumi kupitia fursa za ajira katika sekta ambazo zinaaminiwa kuwa za wanaume.

"Ni kweli kwamba sekta hizi zinazoaminiwa kuwa ni za wanaume, ni sekta zinazokua kwa kasi na zenye fursa nyingi za ajira na kipato. Mfano wa sekta hizo ni pamoja na sekta ya usafirishaji, TEHAMA, maliasili na utalii, uchumi wa bluu/bahari, viwanda na biashara, ujenzi, madini na uziduaji pamoja na nyinginezo.

"Niwapongeze TGNP, Benki ya Maendeleo PLC na Kampuni ya Car & General Trading Ltd kwa mradi huu wa kipekee wa kuwainua wasichana wanaotoka katika mazingira magumu kupata ajira katika sekta hii ya usafiri na usafirishaji kupitia fursa ya kuendesha pikipiki za magurudumu matatu (bajaji)," alisema Dk. Gwajima.

Aliongeza kuwa sekta ya usafiri na usafirishaji Tanzania inaonekana ya wanaume pekee huku jamii ikiwachukulia tofauti wanawake wanaoendesha vyombo vya moto vya umma.

"Nipende tu kuwatoa hofu wanawake kwa kuwathibitishia kuwa hakuna kazi ambayo mwanamke hawezi kufanya, wanawake inabidi tuchangamkie fursa. Tunaweza kufanya kazi yoyote ambayo wanaume wanafanya," alisema.

Dk. Gwajima alisema kuwa wasichana 10 ambao wamepewa bajaji wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya uwezeshwaji kiuchumi kwa takribani mwaka mmoja na nusu kwa awamu ya kwanza na wanaandaliwa wengine mikoani.

"Nimeambiwa pia kuwa mradi huu ulifadhiliwa na Ubalozi wa Australia, kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu wasichana 50 waliweza kufaidika na fursa za mafunzo ya udereva na wasichana 20 waliweza kujifunza uchomeleaji.

"Nimefurahi kusikia kuwa mradi huu ulitoa pia fursa zaidi, baada ya mafunzo ya awali ya udereva walipewa pia fursa ya kuendelea kujifunza kuendesha magari ya magurudumu matatu na wengine kuendesha 'folk lifts' na malori," alisema Dk. Gwajima.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi,

alisema Mradi wa Pink Ride ni programu ya mafunzo ya udereva wa bajaji kwa wasichana unaoendeshwa na TGNP, Car & General na Maendeleo Bank.

Alisema mradi huo unalenga kuongeza mapato ya kiuchumi ya wanawake vijana kutoka kwa familia zilizo na uwezo wa chini na kupambana na unyanyasaji wa kijinsia kwa wasichana/wanawake unaotokana na ukosefu wa kipato.

"Bajaji 10 watakabidhiwa kama mkopo na utalipwa na wasichana hawa. TGNP, Maendeleo Bank na Car & General (C&G) wameshirikiana katika uwezeshaji na utoaji wa mafunzo ya kijinsia na malipo ya mkopo, ili kuhakikisha wasichana hawa wanatimiza ndoto zao.

"Vyombo hivi vimefungwa mfumo wa mawasiliano na baadaye vitaunganishwa na huduma za usafiri mitandaoni," alifafanua.

Mkurugenzi Mtendaji wa Maendeleo Bank, Ibrahim Mwangalaba, alisema benki hiyo imetoa mikopo ya bajaji kwa wasichana hao kupitia mradi wa Pink Ride ambao utapanuliwa katika mikoa mingine siku zijazo.

"Bajaji hizi tulizozitoa leo (juzi) zina thamani ya Sh. milioni 84 ambapo ifikapo Desemba mwaka huu tunatarajia kutoa bajaji 500 zenye thamani ya Sh. bilioni nne," alisema Mwangalaba.

HABARI KIMATAIFA

## Putin: Russia ina mabomu ya kutosha

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, amesema nchi yake ina shehena ya kutosha ya mabomu ya mtawanyiko ya kujibu mashambulizi ikiwa Ukraine itatumia silaha kama hizo kuwashambulia wanajeshi wake wanaopigana Ukraine.

Rais Putin aliyasema hayo katika mahojiano yaliyochapishwa jana na televisheni ya taifa hilo, akieleza kuwa, bado bado Russia haijatumia aina hiyo ya silaha licha ya kuwa na uhaba wa mabomu kwa kiasi fulani.

Inaelezwa kuwa awali Ukraine ilianza kupokea mabomu ya mtawanyiko kutoka Marekani, hali ambayo imesababisha wasiwasi kutokana na athari za muda mrefu zinazotokana na matumizi ya mabomu hayo kwa raia.

Pia inabainishwa kuwa sehemu ya aina hiyo ya mabomu yanayoshindwa kulipuka papo hapo, yanaweza kusababisha hatari miongo mingi baadaye hasa kwa watoto.

Shirika la haki za binadamu la Human Rights Watch na majeshi ya Ukraine yameituhumu Russia kuwa tayari inatumia mabomu ya mtawanyiko kwenye uwanja wa mapambano na kwamba mabomu hayo, yalipigwa marufuku kutumika kwa karibu nchi 100.

Nchi hizo ni zile zilizotia saini azimio la Oslo la mwaka 2008, na kwamba Russia na Marekani siyo sehemu ya mkataba huo, huku makundi ya haki za binadamu yakilaani uamuzi wa Marekani wa kupatia Ukraine mabomu hayo.

Licha ya lawama hizo, Rais wa Marekani, Joe Biden, alisema kuwa uamuzi huo ulikuwa mgumu, akisisitiza kuwa Ukraine inahitaji mabomu ya ziada ili kuijaza tena hifadhi yake iliyopungua.

Hata hivyo, Russia ilieleza kwamba imezidungua takriban droni 10 kwenye mji wa Sevastopol katika rasi ya Crimea ambayo iliinyakua kutoka kwa Ukraine mwaka 2014.

Wizara ya ulinzi ya Russia ilieleza kwamba jeshi la ulinzi wa anga liliziangusha ndege mbili zisizo na rubani na kuzizima nyingine tano. **DW**

## 35 wauawa mafuriko Korea Kusini

**SEOUL,** KOREA KUSINI

WATU 35 wamepoteza maisha Korea Kusini baada ya mafuriko na maporomoko ya ardhi, huku ikielezwa kuwa wengine zaidi ya 10 hawajulikani waliko.

Inaelezwa kuwa waokoaji wanaofanya kazi ya kuyafikia magari yaliyokwama kwenye handaki au njia ya chini ya magari iliyofurika

maji karibu na mji wa Cheongiu nchini humo wamefanikiwa kupata miili tisa.

Inaelezwa kuwa bado haijabainika ni watu wangapi wamenasa kwenye handaki hilo lenye urefu wa mita 685 katika mji wa Osong, lakini magari 15 yanakisiwa kuzama, na kwamba miili kadhaa iliopolewa kutoka ndani ya basi.

Inabainishwa kwamba maji ya mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa ya siku kadhaa yalimwagika kwa kasi kwenye njia ya chini kiasi cha abiria na madereva kunaswa kwenye magari yao, na kushindwa kutoka.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa watu tisa walionusurika waliokolewa, huku vifo vingi vikiripotiwa Gyeongsang Kaskazini, eneo ambalo maporomoko ya ardhi yaliporomosha nyumba nzima.

# Ramaphosa, Putin wajadili kuongeza muda wa usafirishaji wa nafaka

**CAPE TOWN,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa na mwenzake wa Russia, Vladimir Putin, wamejadili mustakabali wa makubaliano ya kuongeza muda wa usafirishaji nafaka katika bahari nyeusi, makubaliano ambayo yanaruhusu Ukraine kusafirisha ngano yake kutoka bandari zake, licha ya vita.

Inaelezwa kuwa muda wa usafirishaji uliowekwa awali unakamilika leo jioni, huku Kremlin ikieleza kuwa Rais Putin amemkumbusha mpatanishi wake Rais wa Afrika Kusini kwamba maombi ya Russia ya kuondoa vikwazo kwa mauzo yake ya mbolea na bidhaa za chakula hadi sasa hayajaheshimiwa.

Mazungumzo hayo yaliyofanyika jana kwa njia ya simu yanakuja baada ya taarifa za Rais wa Uturuki, Recep Erdogan, ambaye alisema kuwa mwenzake wa Russia anakubali kuendeleza eneo salama la kupitisha nafaka katika Bahari Nyeusi.

Aidha, inaelezwa kuwa Ramaphosa anatarajia kuendeleza majadiliano, pia na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, ambaye tayari alikuwa akizungumza naye wiki iliyopita, pamoja na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres.

Ilielezwa kuwa ikiwa makubaliano hayo hayatarefushwa tena, Afrika inaweza kukabiliwa na hali ngumu na kuona usalama wake wa chakula ukiwekwa katika hatari zaidi.

Marais wa Afrika Kusini na Russia pia wamejadili mkutano wa kilele wa BRICS (Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini), utakaofanyika mwishoni mwa mwezi Agosti huko Johannesburg, bila kutajwa kwa sasa ikiwa Rais Putin atashiriki au la mkutano huo.

**RFI**



Maji ya mafuriko yakiwa yamejaa mbele ya makazi ya wananchi huko Korea Kusini baada ya mvua kubwa kunyesha, ikielezwa kuwa huenda idadi ya vifo vinavyotokana na mafuriko hayo vitaongezeka. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Ruto amshutumu Kenyatta kuunga mkono maandamano

**NAIROBI,** KENYA

RAIS wa Kenya, William Ruto, amemwonya mtangulizi wake Uhuru Kenyatta kwa madai ya kuendelea kushirikiana na kiongozi wa upinzani Raila Odinga.

Rais Ruto, akizungumza katika mji wa Mai Mahiu kaunti ya Nakuru, kwenye mkoa wa bonde la ufa, alieleza kuwa Kenyata amekuwa akifadhili kwa siri maandamano ya Odinga dhidi ya serikali ambayo hivi majuzi yaligeuka kuwa vurugu huku vifo vingi vikiwa vimerekodiwa.

Inaelezwa kuwa hayo yamejiri wakati huu Rais Ruto akimtahadharisha Odinga dhidi ya kuendelea na maandamano yake yaliyopangwa kufanyika kwa siku tatu kuanzia wiki hii, akisema serikali itamchukulia hatua kali iwapo atafanya hivyo.

Pia Rais alionya kwamba, ingawa kufanya maandamano ni haki ya raia yeyote kama ilivyoainishwa katika katiba, Odinga atakabiliwa vikali na vyombo vya usalama iwapo umwagaji damu zaidi utashuhudiwa katika mchakato huo.

Ruto aliapa kumkabili kikamilifu Odinga kisiasa na kuhakikisha kwamba anastaafu na kurejea nyumbani kwake Bondo Magharibi ya Kenya.

Hata hivyo, aliongeza kuwa iwapo rais wa zamani Kenyatta ataendelea kufadhili maandamano ya Odinga, basi huenda pia atalazimishwa kustaafu na rafiki yake Odinga.

"Nataka nimwambie rafiki yangu Uhuru, ata wewe wachana na huyu mzee (Odinga), wacha kumpatia pesa ya kununua watu wa Mungiki (kundi ambalo limeharamishwa na serikali) wachome Nairobi," alisema Rais Ruto.

"Wewe umekuwa rais, kuwa mungwana, tulikuunga mkono ulikuwa rais wetu, uliunga mtu wa kitendawili mkono tukamwangusha, wachana na yeye," alisema Rais Ruto.

"Usipowachana na yeye, ata wewe tutakusafirisha na huyo kitendawili wako. Uhuru Kenyatta tulimsaidia akiwa Rais, sasa kupanga Nairobi, imemkosea nini," alihoji Rais Ruto.

Vile vile, Rais Ruto alisisitiza kwamba Odinga ndiye aliyesababisha serikali iliyopita, chini ya Uhuru Kenyatta, kushindwa kutimiza ahadi zake kikamilifu, hivyo hatamruhusu kufika popote karibu na utawala wa Kenya Kwanza. **RFI**

# MANDONGA AJA NA NGUMI YA 'NDUKUBE' ULINGONI MWANZA

Na Saada Akida

WAKATI mabondia Watanzania wa Ngumi za Kulipwa, Twaha Kassim 'Twaha Kiduku' na Karim Mandonga, wakitarajia kupanda ulingoni jijini Mwanza Julai 29, mwaka huu, ngumi mpya aina ya 'Ndukube', itashuhudiwa.

Twaha Kiduku atapanda ulingoni kuzichapa na Asamehile Walen kutoka Afrika Kusini pambano la raundi 10 uzito wa Kati lisilo la ubingwa, wakati Mandonga atazichapa na Golala Moses raia wa Uganda.

Akizungumza na Nipashe jana, Mandonga aliwaomba Watanzania ambao wapo karibu na mkoa wa Mwanza kujitokeza kwa wingi kuwapa sapoti kwenye pambano hilo ambalo alijigamba kufanya vizuri.

**"Hii ni mara ya pili nacheza na bondia wa Uganda, Watanzania wategemee burudani yenye viwango vikub wa sasa nimekuja na ngumi mpya inayoitwa 'Ndukube', " alisema Mandonga.**

Kwa upande wa Kiduku alisema amejipanga vizuri kutoa burudani kwa wakazi wa Mwanza na Watanzania kwa ujumla.

"Nimejipanga kucheza vema na bado naendelea na mazoezi, wito wangu kwa Watanzania, waniombea dua nifanye vizuri katika pambano langu," alisema Kiduku.

Promota wa pambano hilo, Kessy Mwambeleko, alisema kutakuwa na mapambano nane ambayo yatachezwa siku hiyo.





Wanafunzi wa Darasa la Saba wa Shule ya St. Anne Marie Academy Mbezi Kimara kwa Msuguri, Dar es Salaam, wakiwaburudisha wageni kwa nyimbo mbalimbali za Bongo Fleva wakati wa mahafali ya 20 ya shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# St. Anne Marie Academy kuibua vipaji

Na Mwandishi Wetu

SHULE ya St. Anne Marie Academy ya Mbezi Kimara kwa Msuguri, Dar es Salaam imeahidi kuendelea kuibua na kukuza vipaji mbalimbali vya wanafunzi wa shule hiyo ili waje kuwa watu maarufu kwenye michezo na sanaa.

Ahadi hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa shule hiyo, Dk. Jasson Rweikiza, wakati wa Mahafali ya 20 ya Darasa la Saba yaliyofanyika shuleni hapo.

Dk. Rweikiza alisema mafanikio ya binadamu hayategemei elimu ya darasani pekee kwa hiyo wameona kuna umuhimu wa kuwaendeleza wanafunzi wenye vipaji vya michezo mbalimbali ili waje kuwa maarufu kama ilivyo kwa wanamichezo mbalimbali.

Alisema walimu wa michezo wa shule hiyo wamekuwa wakifanya bidii kutambua vipaji vya wanafunzi kwenye michezo ya kukimbia, mpira wa miguu, mpira wa kikapu na kucheza muziki.

Alisema katika maboresho wanayofanya kila mwaka shuleni hapo, wamegundua kwamba siyo lazima kila mwanafunzi afaulu masomo ya kawaida kama hesabu, historia, baiolojia na fizikia ili kufanikiwa kwenye maisha.

"Wote mmejionea vipaji walivyoonesha wanafunzi hapa kwa kucheza muziki wa bongo fleva, mitindo mbalimbali ya mavazi na mingine mingi hii inaonesha kwamba kuna vipaji vingi ambavyo tukiviendeleza vinaweza kuwasaidia kupata mafanikio kwenye maisha yao ya baadaye," alisema Dk. Rweikiza.

"Mwanafunzi anaweza kuwa msanii akafanya vizuri na akafanikiwa kimaisha kupitia kazi za sanaa, anaweza kuwa mchezaji mzuri wa mpira na akafanikiwa kupitia kipaji hicho, kwa hiyo kazi kubwa tunayofanya kwa sasa ni kuibua vipaji kwa wenye navyo ili viweze kuwasaidia."

Kwenye mahafali hayo wanafunzi wa shule hiyo walionyesha vipaji vya aina yake kwenye kucheza muziki, kuimba na mitindo mbalimbali ya mavazi ambayo wameibuni wenyewe kwa kushirikiana na walimu wao.

Dk. Rweikiza alisema mwanafunzi anaweza kuwa wa kawaida kwenye masomo, lakini akawa na kipaji ambacho iwapo kitaibuliwa na kuendelezwa anaweza kufika mbali sana na nchi kupata waimbaji wa kimataifa.

Alisema mpango mwingine wa shule hiyo ni kuhakikisha wanafunzi wanafaulu kwa wastani wa alama A kwani uwezo huo wanao kutokana na rekodi nzuri waliyonayo.

## Mashujaa yashusha vyuma, kambi Znz

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Mashujaa FC imetangaza rasmi kuwa itapiga kambi yake mjini Zanzibar kujiandaa na msimu mpya wa mshindano, huku ikiendelea kufanya usajili wa kukiimarisha kikosi chake.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo itakayocheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu ujao, imeeleza kuwa kambi hiyo inatarajiwa kuanza Jumatano wiki hii.

"Tunapenda kuwataarifu kwamba, maandalizi ya msimu ujao kwa klabu yetu yatafanyikia visiwani Zanzibar kuanzia Julai 19," ilieleza taarifa hiyo.

Mashujaa yenye maskani yake Kigoma, ni moja kati ya timu tatu mpya ambazo msimu huu zitacheza Ligi Kuu Tanzania Bara.

Zingine ni JKT Tanzania ambayo ilikuwapo misimu kadhaa iliyopita kabla ya kushuka daraja na sasa imerejea pamoja na Tabora United ambayo ilipanda kwa jina la Kitayosce kabla ya kuamua kubadilisha jina hilo.

Wakati hayo yakiendelea Mashujaa imeendelea kujiimarisha kwa kufanya usajili, ambapo imemsajili kipa aliyewasumbua mno kwenye mechi ya 'play off', Lameck Kanyonga wa Mbeya City, pamoja na kipa mwingine Lukumbiza Pascal kutoka Pamba FC, wengine ni starika Kelvin George kutoka Bumamuru FC ya Burundi, Omari Kindamba, Nassor Kiziwa kutoka Mtibwa Sugar, Abdulnasir Asaa Mohamed 'Gamal' kutoka Mlandege na Adam Adam kutoka Ihefu.

## Kuogelea Taifa kuelekea Japan

Na Shufaa Lyimo

TIMU ya Taifa ya Tanzania kwa upande wa mchezo wa kuogelea inatarajia kuelekea nchini Japan kushiriki mashindano ya Dunia yatakayoanza kutimua vumbi Julai 25-31, mwaka huu, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe juzi baada ya kumalizika kwa semina ya waandishi wa habari za michezo nchini, iliyoandaliwa na Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), Kocha Mkuu wa timu ya Taifa, Alexander Mwaipasi, alisema wamejipanga vizuri kwenda kupeperusha vema bendera ya Tanzania nchini humo.

"Kwa upande wetu tunaamini tutakwenda kuitangaza nchi ya Tanzania kupitia mashindano hayo ambayo yatashirikisha wachezaji kutoka mataifa mbalimbali," alisema Mwaipasi.

Alisema wamefanya maandalizi ya muda mrefu ambayo yatawasaidia kupata matokeo mazuri nchini humo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAGUIRE ATAKIWA WEST HAM
KLABU ya West Ham ina mpango wa kumsajili beki wa kati wa England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 30 kwa mkopo kutoka Manchester United. (***Athletic***)

### DE JONG KUBADILISHWA NA SILVA
KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 26, anaweza kupelekwa Manchester City kama sehemu ya mpango wa kubadilishana utakaomhusisha Mreno Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 28, kwenda Barcelona. (***Mirror***)

### KANE KUTUA BAYERN
RAIS wa heshima wa Bayern Munich, Uli Hoeness, anaamini kwamba mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, atahamia Ujerumani msimu huu wa majira ya joto. (***kicker***)

### VLAHOVIC ATAKIWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur inafuatilia kumnunua mshambuliaji wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic, 22. (***Rudy Galetti***)

### KVARATSKHELIA NA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United imeripotiwa kuweka mezani dau la pauni milioni 82 kumnunua winga wa Napoli mwenye umri wa miaka 22 raia wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia. (***Express***)

### SCOTT OFA MEZANI
WOLVES inatazamiwa kuwasilisha ofa ya thamani ya zaidi ya pauni milioni 20 kumnunua kiungo wa kati wa Bristol City na England, Alex Scott, 19. (***Telegraph***)

### FABINHO ANUKIA SAUDIA
KIUNGO wa kati wa Liverpool na Brazil, Fabinho mwenye umri wa miaka 29, ameachwa kwenye kambi yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Ujerumani kutokana na ofa ya pauni milioni 40 kutoka kwa Klabu ya Saudi Arabia, Al-Ittihad. (***Daily Star***)

### HENDERSON HAKIELEWEKI
NAHODHA wa Liverpool, Jordan Henderson, amekubali maslahi binafsi na Klabu ya Al Ettifaq, lakini bado hakuna makubaliano kati ya klabu hizo mbili. (***Fabrizio Romano***)

### AUBAMEYANG KUTUA MARSEILLE
MCHEZAJI Pierre-Emerick Aubameyang yuko tayari kuondoka Chelsea kwenda Marseille, huku mshambuliaji huyo wa Gabon akiwa tayari kupunguza mshahara wake kufanikisha uhamisho huo. (***Goal***)

### EVANS ATAJWA CELTIC
MLINZI wa kati, Jonny Evans mwenye umri wa miaka 35, ambaye yuko huru, anasakwa na bosi wake wa zamani, Brendan Rodgers, kwa ajili ya kuhamia Celtic. Wawili hao raia wa Ireland Kaskazini walikuwa pamoja kule Leicester City. (***Sun***)

### LUKAKU KUONDOKA INTER
MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30, hatajiunga na Inter Milan baada ya timu hiyo ya Italia kuachana na mpango wake huo, huku Saudi Arabia au klabu nyingine ya Serie A, Juventus zikielezwa kumvutia mshambuliaji huyo wa Chelsea. (***Fabrizio Romano***)

### MAHREZ BADO KWA AL AHLI
WINGA wa Algeria, Riyad Mahrez mwenye umri wa miaka 32, anaendelea kuwa mada ya majadiliano kati ya Manchester City na Al Ahli ya Saudi Arabia. (***Fabrizio Romano***)

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI ATAMBULISHWA KUITUMIKIA INTER MIAMI

**Sasa anatarajiwa kucheza mechi yake ya kwanza Inter Miami Ijumaa wiki hii dhidi ya...**

**MIAMI,** Marekani

LIONEL Messi amesaini rasmi mkataba wa miaka miwili na nusu na Inter Miami CF na jana Jumapili alitambulishwa kwa mashabiki baada ya kujiunga na klabu hiyo kama mchezaji huru akitokea Paris Saint-Germain mwishoni mwa msimu uliopita.

"Tuna furaha kubwa kwamba mchezaji bora zaidi duniani alichagua Inter Miami CF na Ligi Kuu ya soka Marekani (MLS), na uamuzi wake ni ushahidi wa kasi na nguvu nyuma ya Ligi yetu na kukua kwa mchezo huu Amerika Kaskazini," alisema kamishna wa MLS, Don Garber katika taarifa.

"Hatuna shaka kwamba Lionel atauonesha ulimwengu kuwa MLS inaweza kuwa ligi ya chaguo la wachezaji bora zaidi kwenye mchezo. Tunatazamia kuona mechi yake ya kwanza kwa Inter Miami katika mchezo wetu wa Kombe la Ligi baadaye mwezi huu."

Messi hapo awali alitangaza nia yake ya kujiunga na ligi hiyo wakati wa mahojiano yake pamoja na gazeti la Mundo Deportivo na SPORT, akifichua Juni kwamba: "Kuacha soka la Ulaya, baada ya kushinda Kombe la Dunia, ndicho nilichohitaji."

"Nilifanya uamuzi kwamba nitaenda Miami, na tuliamua kuendelea na njia."

Ingawa FC Barcelona walikuwa na uhakika wa kumsajili tena mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 - huku babake Messi, Jorge, akisema kwamba mtoto wake alitaka kurejea katika klabu hiyo ambayo alifunga mabao 672 katika mechi 778 - hali ya kifedha ya klabu ilimsukuma kuchagua Ligi ya Marekani.

"Nilikuwa na ofa kutoka kwa timu nyingine za Ulaya, lakini hata sikuzitathmini kwa sababu wazo langu lilikuwa kwenda Barcelona," alisema Messi.

"Kama jambo la Barcelona halikufanikiwa, basi kuacha soka la Ulaya, zaidi baada ya kushinda Kombe la Dunia, ndicho nilichohitaji. Kumaliza kazi yangu upande huu na kuishi ligi ya Marekani kwa njia tofauti, nikifurahia siku hadi siku na zaidi lakini kwa jukumu lile lile la kutaka kushinda na kufanya mambo vizuri kila wakati, lakini kwa amani zaidi ya akili."

Sasa, Messi anatarajiwa kucheza mechi yake ya kwanza ya Inter Miami Julai 21 wakati wa mechi ya Kombe la Ligi dhidi ya Cruz Azul kwenye Uwanja wa DRV PNK pale Fort Lauderdale, Florida.

Pia ataungana na wachezaji wa zamani wa Barcelona, Jordi Alba na Sergio Busquets, ambao watajiunga rasmi na Inter Miami baadaye wiki hii kwa mazoezi yao ya kwanza.

Watatu hao walicheza pamoja nchini Hispania kuanzia mwaka 2012 hadi 2021, wakishinda mataji matano ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, sita ya Copa del Rey na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wachezaji hao watakuwa chini ya kocha mkuu wa zamani wa Barcelona, Gerardo 'Tata' Martino, ambaye alichukua nafasi ya Phil Neville kama kocha mpya Juni 28.

Ujio wa wachezaji hao unatarajiwa kuiimarisha Miami, kwani ipo nafasi ya mwisho kwenye msimamo wa ligi ya timu za kutoka Mashariki wakiwa na alama 18 tu katika michezo 21 na rekodi ya kushina tano, kupoteza 13 na sare 3.

Timu ina safari ndefu kabla ya kufika hatua ya mtoano ya MLS, ikilazimika kupanda hadi moja ya nafasi tisa za juu kwenye jedwali.

Ligi ya Soka ya Marekani ambayo pia inazihusisha timu kutoka Canada, inachezwa kwa mtindo wa mtoano kutoka pande mbili za Mashariki na Magharibi (Eastern Conference League na Western Conference League) , ambapo bingwa wa kila upande hukutana kwenye fainali na mshindi hubeba kombe, na haina mfumo wa kushuka daraja.

# Ramsey arudi klabu yake ya utotoni

**CARDIFF CITY,** Cardiff

NAHODHA wa Wales, Aaron Ramsey, amerejea katika klabu yake ya utotoni ya Cardiff City kwa mkataba wa miaka miwili, timu hiyo ya Championship ilitangaza jana.

Tangazo hilo limekuja muda mfupi baada ya Nice kuthibitisha kuwa Ramsey ameondoka katika klabu hiyo ya Ufaransa kwa makubaliano ya pande zote mbili.

Kiungo huyo wa kati mwenye umri wa miaka 32, na mchezaji wa zamani wa Arsenal, aliwasili Nice Agosti mwaka jana kwa uhamisho huru na kucheza mechi 34, akifunga bao moja.

Ramsey alicheza kwa mara ya kwanza kwenye kikosi cha kwanza akiwa na umri wa miaka 16 katika Klabu ya Cardiff mwaka 2007, baada ya kufanikiwa kuingia katika akademi ya vijana ya klabu hiyo. Kisha akahamia Arsenal mwaka mmoja baadaye.

"Najisikia ajabu hatimaye kurudi hapa. Siku zote nilifikiri siku moja ningerudi, na sasa ni wakati muafaka kufanya hivyo," alisema Ramsey katika taarifa yake.

"Kwangu ni fahari kuwa sehemu ya timu hii, natumaini kufikia malengo tunayotaka, hakuna hisia bora zaidi kuliko hiyo."

Ramsey, alikuwa nahodha mwenye umri mdogo zaidi kuwahi kutokea katika Timu ya Taifa ya Wales mwaka 2011 akiwa na umri wa miaka 20, na amecheza mechi 82 za kimataifa hadi sasa.

Alikuwa sehemu ya timu ya Wales iliyofika nusu fainali ya Euro 2016 na kushiriki Kombe la Dunia Qatar mwaka jana.







# KANE AKILI YAKE KUTUA BAYERN - RAIS

**MUNICH,** Ujerumani

RAIS wa heshima wa Bayern Munich, Uli Hoeness, ana imani kuwa nahodha wa England, Harry Kane, atahamia klabu hiyo kutoka Tottenham Hotspur msimu huu wa majira ya joto.

Hoeness, rais wa zamani wa Bayern ambaye alirejea hivi majuzi kwa nafasi ya ushauri, aliwaambia waandishi wa habari kwenye kambi ya mazoezi ya timu hiyo Jumamosi kwamba, mshambuliaji huyo tayari ameamua kujiunga na klabu hiyo yenye nguvu ya Bavaria na kwamba mazungumzo na Mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy, yanaendelea.

Hoeness alisema Mjumbe wa Bodi ya Usimamizi, Karl-Heinz Rummenigge na Mtendaji Mkuu, Jan-Christian Dreesen, wamezungumza mara kwa mara na Kane na wawakilishi wake.

"Hadi sasa ilikuwa ni kwamba Harry ameonesha wazi katika mazungumzo yote kwamba mawazo yake yamekamilika. Na ikiwa hivyo ndivyo hivyo, basi tutampata," alisema Hoeness. "Halafu Tottenham italazimika kujitoa."

ESPN iliripoti mapema wiki hii kwamba Kane alitaka kujiunga na Bayern msimu huu wa majira ya joto huku mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, wakifikiria kutuma ofa ya tatu kwa mchezaji huyo.

Spurs wametoa mkataba mpya lakini Kane mwenye umri wa miaka 29, hayuko tayari kuongeza mkataba na klabu hiyo ya Ligi ya Kuu England, kwa mujibu wa ESPN.

Hoeness alisema Tottenham haitaweza kukataa euro milioni 80 au milioni 90 kwa mchezaji huyo, ambaye amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake na Tottenham, na kwamba Kane anataka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tottenham, ambayo ilimaliza katika nafasi ya nane kwenye Ligi Kuu msimu uliopita, haikufuzu kwenye michuano ya Ulaya na Bayern ilishinda Bundesliga.

"Sasa ana nafasi tena ya kuja kwenye klabu kubwa barani Ulaya," alisema Hoeness.

"Tunachopenda sote ni kwamba yeye na mawakala wake, baba yake na kaka, daima wamesimama kwa uwazi na kwa kile wanachokisema."

Hoeness alikubali kuwa mazungumzo na Levy yalikuwa magumu.

"Yeye ni mwerevu," Hoeness alisema. "Yeye hataji bei.

# Fabinho huyo Al Ittihad

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL wamempa Fabinho ruhusa ya kusafiri hadi Saudi Arabia kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na Klabu ya Al Ittihad, kwa mujibu wa 90min.

Kiungo huyo aliondolewa kwenye kikosi cha 'Wekundu' hao kwa ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Ujerumani huku mazungumzo ya uhamisho wa kuelekea Mashariki ya Kati yakizidi kupamba moto.

90min iliripoti Alhamisi kwamba Liverpool walikuwa wamepokea ofa kubwa kutoka kwa mabingwa wa Saudi Pro League, Al Ittihad kwa ajili ya Fabinho.

Na 90min sasa inaelewa kuwa klabu hizo mbili sasa zinakaribia kuafikiana juu ya mkataba wa pauni milioni 40 na Fabinho tayari ameanza kuaga pale Merseyside.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, sasa anatarajiwa kwenda Saudi Arabia kufanyiwa uchunguzi wa vipimo vya afya baada ya kupewa baraka na Wekundu hao kukamilisha uhamisho huo.

Al Ittihad walifanikiwa kuiangusha Al Nassr ya Cristiano Ronaldo na kushinda taji la Saudi Pro League msimu uliopita, huku wakiwaongeza Karim Benzema na N'Golo Kante kwenye safu yao katika dirisha hili la usajili.



Fabinho si kiungo pekee wa Liverpool ambaye anaweza kutimkia Saudi Arabia msimu huu wa majira ya joto, nahodha wa klabu hiyo, Jordan Henderson pia yuko kwenye mazungumzo juu ya uhamisho kama huo.

Kiungo huyo wa kati wa England anatakiwa na Steven Gerrard katika Klabu ya Al Ettifaq, ambao ni miongoni mwa timu chache zenye nguvu ya kifedha.

90min inaelewa kuwa wakati Gerrard anajitahidi sana kufanikisha mpango huo na kukiwa na imani kwamba makubaliano yatafikiwa, Al Ettifaq kwa sasa wanasitasita kufikia bei inayotakiwa na Liverpool ya pauni milioni 20.

Henderson bado hajatoa makubaliano yake ya jumla ya mkataba huo na bado anakadiria ofa hiyo licha ya ripoti kudai kuwa amekubali maslahi binafsi ya kulipwa mshahara wa pauni 700,000 kwa wiki.

HABARI MICHEZO

# KIHIMBWA RASMI MALI YA PRISONS

Na Saada Akida

KLABU ya Tanzania Prisons, imefanikiwa kuinasa saini ya kiungo wa Mbeya City, Salum Kihimbwa, kwa mkataba wa miaka miwili kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/24.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa timu hiyo, Enock Manguku, alisema mchakato wa usajili unaendelea vizuri kwa kuzungumza na baadhi ya wachezaji kushirikiana na kocha wao, Freddy Felix Minziro.

Alisema wakati wakiendelea kufanya usajili wanazingatia zaidi mipango yao kwa kuangalia vigezo vyao vya usajili kwa kuwapa nafasi kubwa wachezaji vijana zaidi kuimarisha kikosi cha timu yao.

"Hawa wanaoacha na hizi klabu kubwa Simba, Yanga na Azam FC, si kipaumbele chetu kikubwa, kwa sababu tunahitaji watu ambao wanataka kupigania ndoto zao na kucheza soka safi.

"Hatusemi kwamba hatutawachukuwa ila malengo yetu ni kuwapa nafasi vijana ila tukiwapata waliotoka katika timu hiyo basi tutaangalia ambao wanaendana na mfumo wa timu yetu," alisema Manguku.

Aliongeza kuwa kikosi cha timu hiyo tayari kimeshaanza maandalizi ya msimu ujao kwa wachezaji kukutana kwenye maskani yao jijini Mbeya kabla ya Agosti Mosi, mwaka huu kuelekea kambini visiwani Zanzibar.







Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), James Mbalwe, akionyesha Tuzo ya Mshindi wa Kwanza Kundi la Mamlaka za Usimamizi (Regulatory Boardies) kwenye Kilele cha Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# GBT yatwaa tuzo ya mamlaka bora ya usimamizi

Na Mwandishi Wetu

BODI ya Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha Tanzania (Gaming Board of Tanzania - GBT), imetwaa tuzo ya mshindi wa kwanza (First winner prize), katika Kundi la Mamlaka za Usimamizi (Regulatory Bodies) kwenye Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyofikia kilele Julai 13, mwaka huu.

TanTrade iliweka utaratibu mpya wa namna ya kumpata mshindi ambapo mwaka huu wananchi ndio waliopewa fursa ya kuchagua mshindi kwa kupiga kura kupitia mtandao tofauti na miaka ya nyuma ambapo kamati maalum ilikuwa ikipita kwenye mabanda kisha kuchagua washindi.

"Sisi tunachukulia haya ni mafanikio makubwa sana kwetu na tunawashukuru Watanzania kwa kututambua na kuthamini kazi nzuri inayofanywa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT)," alisema Mkurugenzi Mkuu wa GBT, James Mbalwe, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Alisema wananchi wanatambua mchango wa sekta ya michezo katika maendeleo ya nchi.

"Katika mwaka huu wa fedha ulioishia Juni 2023 kiasi cha shilingi bilioni 160 za kodi ya moja kwa moja zitakusanywa kutoka kwenye sekta ikiwa ni ongezeko la kiasi cha shilingi bilioni 148 zilizokusanywa katika mwaka wa fedha uliopita 2022," alifafanua.

Alisema GBT itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo kwani michezo ya kubahatisha ni burudani sio ajira, ila ni ajira kwa waendeshaji na burudani kwa wachezaji.

Alisema GBT imefikisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwake na kadiri muda unavyokwenda ndivyo imekuwa ikiimarika zaidi.

Akifafanua zaidi kuhusu tuzo, Ofisa Uhusiano Mwandamizi GBT, Zena Athumani, alisema mbali na kupata tuzo hiyo ya mshindi wa kwanza Kundi la Mamlaka za Usimamizi, GBT pia ilitwaa tuzo ya mshindi wa tatu wa Banda Bora la Maonesho mwaka huu.

## Chama, Che Malone waifuata Simba...

INATOKA UK 24

ambaye ataungana na timu hiyo akitokea nchini kwao Senegal.

"Nyota hao wanaondoka kwenda kuungana na jeshi letu Uturuki, viongozi tukiendelea na mipango yetu na kuelekea Moshi kwa ajili ya kwenda kupanda Kilele cha Mlima Kilimanjaro kutambulisha jezi yetu ya msimu.

"Wengi wanadhani tumeamua kuzindua jezi juu ya Mlima Kilimanjaro kwa lengo la kujibu mapigo ya wale waliogawa jezi Lilongwe. Kwa miaka sita sasa tumekuwa tukibeba bendera ya utalii wa nchi kupitia Visit Tanzania," alisema Ahmed na kuongeza:

"Sisi tunaamini tunaowajibu wa kusaidia serikali yetu kutangaza utalii wetu, tangu tumetangaza kuzindua jezi juu ya Mlima Kilimanjaro, taarifa imesambaa dunia nzima na kila mmoja anahamu ya kushuhudia tukio hilo."

Alisema kuzindua jezi juu ya mlima huo ni tukio la kwanza duniani na dunia nzima inasubiri kushuhudia itakuwaje wakati wa uzinduzi huo kwa kushuhudia uzuri wa Mlima Kilimanjaro, baada ya hapo watakuwa wametimiza malengo.

Leo viongozi hao wa 'Wekundu wa Msimbazi' wanaondoka kuelekea Moshi na Jumatano kuanza zoezi la kupanda mlima huo kwa ajili ya Ijumaa kuzindua jezi hizo rasmi kwa mashabiki kuona uzi wao mpya wa msimu wa 2023/24 ambao utakuwa madukani kote nchini kuanzia Jumamosi wiki hii.

## Mazoezi ya Yanga Kigamboni usipime

INATOKA UK 24

Kuhusu mikakati yake, Hafidh alisema kocha wao aliwasisitizia watu wote walio kwenye benchi lake la ufundi nidhamu na ushirikiano.

"Kocha alituita akatuambia mikakati yake, anachozingatia ni nidhamu na ushirikiano, anasema tumechukua makombe mara mbili na fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, kwa hiyo timu 15 zilizo nyuma yetu zitakuwa zimepania kutuondoa kwenye utawala kwa hiyo lazima tushirikiane, wachezaji wawe na nidhamu na yeye tumpe ushirikiano, tunaweza kusonga mbele," alisema.

Yanga imeanza mazoezi yake ikiwa na kocha mpya, pamoja na baadhi ya wachezaji watano mpaka sasa iliyowasajili kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano.

Wachezaji hao ni Kouassi Attohoula Yao, beki wa kulia, raia wa Ivory Coast, akitokea Klabu ya Asec Mimosas ya nchini humo, Maxi Mpia Nzengeli kutoka Maniema FC ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, beki wa kati raia wa Uganda, Gift Fred kutoka SC Villa ya Uganda, Nickson Kibabage akitokea Singida Fountain Gate, na Jonas Mkude ambaye aliachwa na Klabu ya Simba.

Michezo
Nipashe Jumatatu Julai 17, 2023



UK. 21

Messi atua rasmi Inter Miami

# Chama, Ngoma waifuata Simba Uturuki

●●● Wamo pia Che Malone, Onana na Kramo, kocha asema kambi imenoga, asifu...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha wa viungo wa Simba, Corneille Hategekimana, akisifu kambi ya timu yao Ulaya kuwa nzuri na wachezaji wake kuimarika kwa haraka, nyota wengine ambao walibakia nchini kwa sababu mbalimbali, wanakwea pipa leo kwenda Uturuki kuungana na wenzao kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya, imeelezwa.

Wachezaji ambao walibaki nchini kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuchelewa kupata visa ni pamoja Jean Baleke, Willy Essomba Onana, Che Fondoh Malone, Aubin Kramo, Fabrice Luamba Ngoma na Clatous Chama ambaye alikuwa na matatizo binafsi pamoja na Pape Sakho, aliyekuwa kwao Senegal.

Akizungumza na gazeti hili jana Hategekimana alisema wamepata sehemu nzuri yenye ubora mkubwa wa kufanya maandalizi na tangu wamefika nchini humo ni siku nne ambazo wamefanya mazoezi na wachezaji wameonekana kuelewa na kuimarika haraka.

Alisema licha ya kutokamilika kwa wachezaji wote ndani ya kikosi hicho, anaimani kubwa mwisho ya 'Pre Season' hiyo watakuwa vizuri zaidi, kiutimamu wa mwili, kiufundi na mbinu za uwanjani.

"Tangu tumefika hapa tulifanya mazoezi ya viungo gym , tukaenda kwenye bwawa la kuogelea ambalo kuna mazoezi yake ni muhimu kwa kumjenga mchezaji utimamu wa mwili na tumekuwa na programu ya uwanjani kwa kocha Robertinho [Oliveira], alianza kufanya majukumu ya mbinu na ufundi [kabla ya kurejea kwao Brazil kwa muda].

"Tuko na timu nzuri sana wachezaji wameonyesha kuelewana vizuri kwa kile kinachotolewa kutoka kwetu wanajua nini wanatakiwa kufanya wanapokuwa na mpira au hawana, jinsi ya kujilinda na mpinzani, huko mbele kutakuwa na kazi kubwa kwa wapinzani wetu," alisema Hategekimana.

Kwa mujibu wa Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, jana alisema baadhi ya wachezaji wanaondoka leo kuelekea nchini Uturuki kujiunga na wenzao kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano.

Aliwataja wachezaji hao ni Baleke, Chama, Onana, Che Malone, Kramo, Ngoma na Sakho

INAENDELEA UK 23



Chama

# Mazoezi ya Yanga Kigamboni usipime

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga tayari wameanza kambi na mazoezi ya kuanza kwa msimu mpya 'pre season' maeneo ya Kigamboni huku Kocha Mkuu, Miguel Angel Gamondi, akija na mbinu mpya ya kuwapa stamina na kuchezea mpira kwa wakati mmoja.

Mratibu wa Klabu hiyo, Hafidh Salehe, alisema jana kuwa kocha Gamondi kama wengine na yeye amekuja na mpango mkakati wake wa kuwataka wachezaji kwanza kuuchezea mpira uwanjani, halafu baadaye anaanza mazoezi ya kuwajaza pumzi na stamina, hasa ikizingatiwa kipindi hiki ambacho wachezaji wametoka mapumzikoni.

"'Pre season' kila mwalimu ana mbinu zake, zamani miaka hiyo wachezaji mkirejea kutoka kwenye mpumziko ni mbio tu kama wiki nzima hakuna kugusa mpira, walimu wanajenga stamina na pumzi kwa sababu wachezaji walikuwa mapumzikoni miili imejaa, makocha zamani walikuwa wanaona hiyo ni mbinu pia ya kuwapunguza uzito kwani baadhi yao wanakuwa wamenenepa, baada ya wiki moja ndiyo watu wanagusa mpira, mazoezini na katika mechi za kirafiki," alisema mratibu huyo.

Hata hivyo, alisema kwa sasa soka limebadilika duniani kote na kila kocha anakuja na mbinu zake mpya za ufundishaji inapoanza 'pre season.'

"Sasa hivi soka limebadilika sana kama unavyoona mwalimu wetu mpya amekuja na staili ya kuacha wachezaji wanacheza soka kidogo, halafu wanajaza pumzi, kama nilivyotangulia kusema kila tunapozidi kusonga mbele, soka duniani linabadilika," alisema mratibu huyo wa siku nyingi kwenye klabu hiyo.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >